
BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,021,208,577/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

## Rais Samia ataka hatua uharibifu wa mazingira nchini



## Tierney wa Arsenal awindwa Man City

UKURASA 22

Nipashe
Jumamosi Agosti 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581036
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# 'Gonjwa' latafuna mamilioni ya nchi

**Hospitali** moja yatumia mil 500/- kwa mwaka... *Uk. 2*

UKURASA 7

### CCM: UCHAGUZI UTARUDIWA TUKIBAINI WAMEPANGA SAFU

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema atafuta uchaguzi wa ndani wa chama kwa maeneo ambako itabainika kuna wanachama waliopanga safu ya uongozi kwa maslahi binafsi...

UKURASA 15

### UGUMU WA MAISHA KIINI KUKATISHA ARV

LICHA ya kuongezeka kwa kiwango cha kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa wanaoishi na virusi hivyo (WAVIU) wanaotumia dawa kutoka asilimia 87 mwaka 2016 hadi asilimia 92 mwaka 2019, hali duni ya maisha imetajwa kuwa moja ya vikwazo vinavyochangia...

## Mbaroni tuhuma kutorosha dhahabu

UKURASA 2




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha fedha Sh.milioni 97.2 kwa waandishi wa habari, mkoani humo jana, baada ya kuwakamata watu sita wakitorosha madini ya dhahabu ya uzito wa Gramu 930.88 yenye thamani ya Sh. milioni 93, kwenda kuuza nje ya nchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Vurugu zaibuka katika ukumbi majumuisho ya kura Kenya

UKURASA 3

MICHEZO LAZIMA TUWACHAPE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa zawadi ya picha maalum iliyotengenezwa na vijana wa Zanzibar, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, wakati wa maadhimisho ya kilele cha Siku ya Vijana Kimataifa, jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# 'Gonjwa' latafuna mamilioni ya nchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amebaini kuwapo kwa ongezeko la wagonjwa kutoka katika migodi ya madini ambao wanaathirika na vumbi linalotokana na shughuli za uchimbaji huku baadhi yao wakipumulia mashine kwa zaidi ya miaka miwili.

Amesema utafiti uliofanywa kwenye migodi 22 ya Mirerani wilayani Simanjiro, umeonyesha kiwango cha silica kwenye vumbi linalovutwa na wachimbaji kilikuwa cha wastani wa miligramu 1.227, kiwango ambacho ni kikubwa zaidi ya mara 25 ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha miligramu 0.05.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mpango ameagiza Wizara ya Madini ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Wizara ya Afya kuhakikisha sheria na kanuni za afya na usalama mahala pa kazi zinafuatwa na kuweka utaratibu wa haraka wa kudhibiti baa hilo.

Pamoja na hayo, ameagiza kuongezwa kwa kasi ya ukaguzi wa migodi mikubwa na midogo ambayo haizingatii uhifadhi wa mazingira ikiwamo kufanya uchafuzi kwenye mito, maziwa na bahari kutokana na matumizi ya kemikali ili kuwachukulia hatua za kisheria.

Kiongozi huyo akizungumza jana kwenye maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la Madini (STAMICO) sambamba na kuzindua nishati mbadala ya mkaa rafiki kwa mazingira (Rafiki Briquettes), alisema katika Hospitali ya Kibong'oto iliyoko Wilaya ya Siha, kwa siku kuna wastani wa wagonjwa 25 waliolazwa, wengi wao wakiwa vijana kati ya miaka 20 na 40, ambao wameathirika na vumbi hilo.

"Wagonjwa hawa wanatumia takribani mitungi 30 ya hewa tiba ya oksijeni kwa siku na hivyo kugharimu serikali zaidi ya Sh. milioni 500 kwa mwaka kwa hospitali hii moja tu, baadhi yao wapo hospitalini pale kwa zaidi ya miaka miwili wakipumulia mashine," alisema. Dk. Mpango alisema vumbi hilo limekuwa likiathiri mfumo wa upumuaji na kusababisha ugonjwa wa 'silicosis' inayosababisha mapafu na madhara yake ni pamoja na kupata saratani ya mapafu, kufeli kwa figo na moyo.

"Pia ni kichocheo kikubwa cha maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu ambao ni tishio kwa taifa letu, utafiti uliofanywa kwa wachimbaji 330 katika migodi ya mirerani mwaka 2021, matokeo ya awali yanaonyesha wachimbaji 99 sawa na asilimia 30 walikuwa wameathirika na ugonjwa wa silicosis na wachimbaji 20 sawa na asilimia 6.1 walikuwa na ugonjwa wa kifua kikuu, hii ikiwa ni mara 24 zaidi ya wastani wa kitaifa," alisema.

**NAMNA YA KUJIKINGA**

Aliagiza elimu kwa wamiliki wa migodi na wachimbaji kuhusu namna bora ya kujikinga na vumbi wanapokuwa katika shughuli za uchimbaji wa madini ikiwamo uvaaji wa barakoa na unyunyiziaji wa maji ili kupunguza vumbi.

"Ninawataka Tume ya Madini kusaidia fedha na vitendea kazi ili kuboresha afya za wachimba madini. Vilevile, Wizara ya Madini na wakuu wa mikoa yote yenye migodi ya madini nchini, viongozi wa chama cha wachimbaji pamoja na wamiliki wa migodi ninawashauri mkatembelee Hospitali ya Kibong'oto kujionea hali ilivyo.

"Ninaamini mkijionea vijana wetu wanavyoteseka, mtaguswa na kuchukua hatua madhubuti," Dk. Mpango aliagiza.

**KIBANO MASHIRIKA**

Makamu wa Rais pia aliyataka mashirika mengine ya umma ambayo utendaji wao unasuasua, kuchukua tahadhari mapema ya kujikwamua.

"Serikali inaendelea kufanya tathmini ya mashirika yanayojiendesha kwa hasara na itachukua hatua stahiki kulingana na taarifa ya tathmini inayofanyika.

"Hivyo, ninawashauri mjipange kabla hamjapangwa! Mzaliwe upya na viongozi wa taasisi zinazofanya vizuri kwa kipindi cha kuridhisha, serikali inawaona na watapata tuzo wanayostahili," alisema.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alisema pamoja na STAMICO kupitia kipindi kigumu, kwa sasa wanajitegemea wenyewe na jana walitoa gawio kwa serikali la Sh. bilioni 2.2. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, aliitaka STAMICO kuongeza uzalishaji wa mkaa huo mbadala ili kukidhi mahitaji ya Watanzania.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema shirika limefanikiwa kufufua mgodi uliokuwa umesimama tangu mwaka 2012 ambapo uzalishaji unaendelea na hivi karibuni waliingia mkataba wa kuuza makaa ya mawe tani 60,000 nje ya nchi na hivyo kuliingizia shirika Sh. bilioni 4.16 kwa mwezi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Seif Gulamali, alisema mwaka 2018, STAMICO ilikuwa ikiyumba lakini kwa sasa inazalisha zaidi ya Sh. bilioni 48, hivyo wamefanya mapinduzi makubwa kwa muda mfupi.

Mkurugenzi wa Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina, Lightness Mauki, alisema shirika hilo ni miongoni mwa mashirika 237 ambayo serikali imeweka uwekezaji wake na kwa sasa linatengeneza faida.

# Mbaroni tuhuma za kutorosha dhahabu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limewakamata watu sita kwa tuhuma za kutorosha madini ya dhahabu katika Barabara ya Ilogi wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Watu hao wamekamatwa wakiwa na madini yenye uzito wa gramu 930.88 yenye thamani ya Sh. milioni 93 huku wakiwa na fedha Sh. Milioni 97.2 kwenye begi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa watu hao walikamatwa Agosti 10, mwaka huu, majira ya saa 3:00 usiku.

Alisema, askari polisi wakiwa katika doria ya kawaida, waliwasimamisha watu hao wakiwa na gari aina ya Toyota lenye namba T.913 DRX katika barabara ya Ilogi kwenda mkoani Geita.

Kwa mujibu wa kamanda magomi, baada ya kuwasimamisha na kuwapekua, waliwakuta na madini hayo pamoja na fedha kwenye begi.

"Wakati wa upekuzi wa gari hilo, tulifanikiwa kukuta madini ya dhahabu yenye uzito wa gramu 930.88 yenye thamani ya Sh. milioni 93, pesa taslimu Sh. milioni 97, mzani mmoja wa kielektroniki wa kupimia dhahabu na mashine moja ya kupima ubora wa dhahabu," alisema Magomi.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa watuhumiwa walikuwa wakitorosha madini haya kwenda nje ya nchi kwa lengo la kukwepa kilipa kodi na tozo za serikali kitendo ambacho ni kosa kisheria," aliongeza.

Pia, alisema taratibu za kipolisi zinaendelea kufanyika na zitakapokamilika watuhumiwa watafikishwa kwenye mahakamani, huku akitoa wito kwa wananchi hasa wanaojihusisha na biashara za madini wafuate taratibu zote za uuzaji wa madini hayo.

# Pacha mwingine waliotenganishwa afariki dunia MNH

**Na Romana Mallya**

PACHA waliotenganishwa kwa operesheni katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Neema na Rehema, wamefariki dunia wote wakipishana siku 33.

Baada ya operesheni hiyo kufanyika Julai Mosi mwaka huu, siku 10 baadaye (Julai 10) Neema alifariki dunia na juzi (Agosti 11) Rehema ambaye alikuwa bado amelazwa kwenye chumba cha uangalizi maalum (ICU) tangu operesheni hiyo ifanyike, naye amefariki dunia.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, alithibitisha jana kufariki dunia kwa pacha huyo, Rehema, aliyefikwa na umauti juzi majira ya saa tano asubuhi.

Julai Mosi mwaka huu, jopo la wataalam 31 wa hospitali hiyo na wengine kutoka nje ya nchi walifanikiwa kuwatenganisha watoto hao waliokuwa wameungana kwa kiwango kikubwa.

Operesheni ya kuwatenganisha ilichukua saa saba ikihusisha kutenganisha ini, mishipa mikubwa na kuitenganisha ngozi iliyopo kwenye moyo.

Neema na Rehema walizaliwa Septemba 21, 2021 kwa njia ya upasuaji wakiwa na kilo 4.9 kwa pamoja katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu na walipewa rufaani kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bungando) na baadaye Muhimbili.

Operesheni ya Muhimbili ilihusisha madaktari wa upasuaji wa watoto wadogo (12), timu ya madaktari wa usingizi (6), madaktari wa kutengeneza uzuri (4), madaktari ambao kazi yao ilikuwa kushughulika na kuangalia mfumo mzima wa mtoto unakwenda vizuri (2) na wauguzi (6).

Upasuaji kama huo ni mara ya tatu kufanyika nchini ambapo wa kwanza ulifanyika mwaka 1994 wa watoto wawili wa kiume waliokuwa wameungana kwenye tumbo.

Wa pili ulifanyika mwaka 2018 ukihusisha watoto wawili wa kiume wanaoishi Kisarawe ambao wana miaka mitatu na miezi 10 sasa na wanaendelea vizuri.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana (katikati) na Mufti Mkuu wa Tanzania, Alhaj Dk. Abubakar Zubeir (kushoto), wakijadiliana jambo na Katibu Mkuu wa Taasisi ya Mohamed VI Foundation, Dk. Sidi Mohamed Rifki, baada ya ufunguzi wa mashindano makubwa ya kusoma na kuhifadhi Quran Tukufu, yaliyoandaliwa na taasisi hiyo, katika Msikiti Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni Muslim, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ISSA MICHUZI**

# Vurugu zaibuka ukumbi wa majumuisho kura urais Kenya

**Na Moshi Lusonzo**

VURUGU ziliibuka usiku wa kuamkia jana katika ukumbi wa Bomas ambao unatumika kujumuisha matokeo ya kura za urais nchini Kenya, baada ya mawakala wa mgombea wa chama cha United Democratic Alliance(UDA) William Ruto, kupandwa na hasira na kutishia kuondoka.

Mawakala hao walipandwa na ghadhabu wakati Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ilipoanza kuhakiki matokeo ya uchaguzi wa urais.

Maofisa wa tume hiyo walionekana kuhangaika kutuliza hali hiyo baada ya mawakala hao kudai kuwa fomu 34A ambazo hazijaidhinishwa ziliingizwa kinyemela katika ukumbi huo.

Hatua hiyo ilisababisha mzozo kutoka kwa mawakala hao waliopandwa na hasira na maofisa wa uchaguzi kuhusu fomu hizo zinazotiliwa shaka. Hata hivyo, makamishna wa IEBC waliingilia kati na kuwatuliza.

Sakata hilo lilianzishwa na Katibu Mkuu wa UDA, Veronica Maina, ambaye alitishia kujiondoa katika mchakato wa kupokea na kukusanya fomu 34A na 34B.

Maina alikuwa akibishana na maofisa wa bodi ya kura kwenye chumba cha kuhakiki kura kabla ya mawakala wengine wa UDA kujiunga nao na mtafaruku huo kudumu kwa takriban dakika 10.

Mawakala wa UDA pia walilalamikia idadi ya watu walioruhusiwa kwenye meza nne zinazotumika kuhakiki na uchukuaji fomu hatua iliyosababisha mkuu wa masuala ya ushirika wa IEBC, Tabitha Mutemi, kuamuru mawakala ambao hawakuidhinishwa kuondoka katika ukumbi huo.

Wakati hayo yakijiri, tume hiyo imesema imeanzisha mchakato wa uhakiki wa ngazi nne na kuashiria matokeo ya nafasi ya urais yatatangazwa leo au kesho.

Kamishna wa Tume hiyo, Prof. Abdi Guliye, alisema tume imeunda madawati manne kwa ajili ya uhakiki wa matokeo kutoka katika majimbo 291 ya uchaguzi yakiwamo magereza na kura zilizopigwa nje ya nchi.

Vituo vya runinga vyasitisha

Katika hatua nyingine, vyombo vya habari nchini humo, vimesimamisha mchakato wa kutangaza matokeo ya awali ya uchaguzi wa rais, hatua iliyoibua maswali juu ya hatima ya uchaguzi huo huku kazi ya kuhesabu kura ikiingia katika siku yake ya nne.

Wachambuzi na waandishi wa habari wa nchini Kenya wameshtuka na kuelezea wasiwasi wao baada ya kugundua kuwa vituo vya televisheni vya KTN, NTV na Citizen vimepunguza kasi au kusimamisha kabisa mchakato wa kuchapisha matokeo ya awali ya uchaguzi wa rais, kadri yanavyoingia.

Kusitishwa kwa matokeo hayo kulifuatiwa na hakikisho la Mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati, kuwataka wananchi kuondoa hofu kutokana na matokeo yasiyofanana yaliyokuwa yakitolewa na vyombo vya habari.

Awali, watu waliingiwa na shaka baada ya vituo hivyo kutoa taarifa za matokeo ya awali yanayokinzana, katika kinyang'anyiro cha urais ambao mgombea wa muungano wa Azimio la Umoja, Raila Odinga anachuana vikali na Naibu Rais, William Ruto anayepeperusha bendera ya muungano wa Kenya Kwanza.

Uchaguzi huo mkuu uliofanyika Jumanne ulifanyika kwa amani, tofauti na uchaguzi wa miaka ya nyuma ambao uliambatana na visa vya ghasia, ambavyo wakati mwingine vilihusisha umwagaji wa damu.

# Samia ataka hatua uharibifu mazingira

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaagiza viongozi wa mikoa, dini na kimila kuhakikisha wanakuja na mpango mkakati wa kutunza vyanzo vya maji na mazingira kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo.

Mkuu wa Nchi pia amewataka wananchi wa Mkoa wa Iringa kuacha kuchoma miti ovyo kwa kuwa wanaharibu mazingira.

Alitoa maagizo hayo jana alipozungumza na wananchi wa mkoa huo kwenye Uwanja wa Samora, akibainisha kuwa mkoa huo una shida ya uendeshaji wa shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji, hasa kwenye mito. "Viongozi wa mkoa wakae na viongozi wa dini, wazee wa kimila na wadau mbalimbali ili kujadili jambo hili na waje na mkakati wa kuhifadhi vyanzo vya maji," aliagiza.

Rais Samia alisema vyanzo vingi vya maji vipo ndani ya Mkoa wa Iringa na ni wajibu wao kuvilinda kwa kuwa ni muhimu kutokana na miradi ya mikakati inayoendelea nchini. "Nimemsikia Waziri wa Maliasili na Utalii toka tumeanza Njombe kuja Iringa anazungumzia hili la kuchoma miti, ndugu zangu tupunguze kuchoma miti, tunaharibu misitu yetu," aliagiza.

Aliagiza kufanyika upandaji wa miti ili kukabiliana na ukataji wa miti kwa ajili ya mbao, akibainisha kuwa sasa kuna ongezeko la wawekezaji wengi katika eneo hilo.

Alisema Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa iliyopata fedha za serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kwa mwaka wa fedha 2022/23 ilipatiwa Sh. bilioni 236.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

"Mkoa wa Iringa ni mkoa wa kilimo, asilimia 75 ya wananchi wanategemea kilimo, sote tunatambua chakula kinachozalishwa kwa wingi katika mkoa huu kinalisha mikoa mingine," alisema.

Alisema wako katika mchakato wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa skimu ya umwagilijai katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo. "Ujenzi wa skimu utakapokamilika, utaongeza hekta 9,075 za umwagiliaji na kufanya jumla ya hekta 24,811, sawa na asilimia 48.2 ya eneo lote linafaa kwa umwagiliaji. Ujenzi wa miradi hii unatarajia kuanza Septemba mwaka huu na rai yangu kwa wananchi ni kuendelea kutumia miradi mipya ya umwagiliaji maji na kuitunza kwa manufaa ya kizazi kijacho,"aliagiza, akigusa pia utatuzi wa migororo ya ardhi.

Rais Samia alisema mkoa huo una hifadhi nzuri za kihistoria na kutokana na umuhimu wa rasilimali hizo, serikali imechukua hatua ya kuufungua kiuchumi kwa kujenga barabara, kiwanja cha ndege na kutenga eneo kwa ajili ya kuwekeza hoteli kubwa na shughuli zingine za kitalii.

**BEI YA SARUJI**

Katika hatua nyingine, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amemtaka Ofisa Biashara Mkoa wa Mara kuwasaka na kuwahoji mawakala wa saruji wanaouza kwa Sh. 27,000 kinyume cha taratibu zilizowekwa.

Alisema bei elekezi ya saruji ni 14,000 hadi 16,000 nchi nzima na 22,500 kwa Mkoa wa Mara.

"Mawakala wote waliopandisha bei ya saruji katika Mkoa wa Mara wakamatwe na kuhojiwa, haiwezekani wakiuke bei elekezi na wawaumize wananchi, ninakuagiza Ofisa Biashara watafutwe na kuhojiwa," aliagiza.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema mkoa huo utahakikisha unadhibiti mianya yote ya upotevu wa fedha za serikali.

■**Imeandaliwa na Martha Sambo (IRINGA) na Beatrice Shayo (DAR)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA)**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(THE JUDICIARY)**
**MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA KAZI**
**LABOUR DIVISION OF THE HIGH COURT)**

**(Rule 16)**
**Samansi**
**(Summons)**
***(Made under Labour Court Rules, Rule 16 GN.106/2007 and O.V, R. I & 2 of CPC Cap 33 RE 2002)***

**REVISION....Na..112 ya Mwaka 2022...................**
***(Complaint/Appeal/Application/Review/Revision/Referral (Reference) No. ..........of year............)***
**Baina ya**
**(Between)**

**SIMBANET TANZANIA LTD.......................................................Mlalamikiwa/Mwombaji -(Applicant)**
**Na**
**AGNES MWAMBO .................................................................Mlalamikiwa/Majibu Mambi - (Respondent)**

KWA;
AGNES MWAMBO
DAR ES SALAAM

Unatakiwa kufika binafsi mbele ya Mahakama hii ikikaa **DAR ES SALAAM** mnamo tarehe **6 Mwezi SEPTEMBER Mwaka 2022 saa 6.00 Mchana.** Mbele ya **Mhe.A.RWIZILE, J** na kubakia Mahakamani hadi uruhusiwe na Mahakama kuondoka, kwa ajili ya kutajwa/kusikilizwa kwa **marejeo/maombi/mgogoro/denituzo na unatakiwa kujibu hati ya kiapo ndani ya siku kumi na tano (15).**
*(You are required to appear in person before this Court at .... On the ..... day of ....20...... at (time).....*
***Before Hon.............*** *and to remain in attendance until permitted by the Court for mention/hearing* of revision. ***Miscellaneous/dispute/execution and file counter affidavit within fifteen days (15)***
Na unatahadharishwa kuwa usipuuze asilani kutii samansi hii vinginevyo utaadabishwa kwa kutozwa faini au kufungwa jela.
(You are further cautioned that you shall on no account neglect to comply with this summons lest you render yourself liable to a fine or Imprisonment).

Imesainiwa hapa .....**DSM**... siku **JUMATANO tarehe 3 mwezi 8 Mwaka 2022**
***(Signed at) ....................(today this.........(day of......20........***




216987102

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF ENERGY

ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (EWURA)

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

# TANGAZO KWA UMMA

## MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA

Mnamo tarehe 19 June 2022 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za huduma za maji safi na usafi wa mazingira kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea. Majedwali Namba 1 hadi 5 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea.

**Jedwali Na. 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Matumizi (Mita za Ujazo) | Bei ya Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 0-10 | 1,110 | 1,740 | 1,850 | 1,880 |
| | 10<25 | 1,200 | 1,880 | 2,000 | 2,030 |
| | >25 | 1,240 | 1,940 | 2,060 | 2,100 |
| Taasisi | 0-20 | 1,145 | 1,940 | 2,060 | 2,100 |
| | >25 | 1,240 | 1,940 | 2,060 | 2,100 |
| Biashara | 0-10 | 1,240 | 2,080 | 2,210 | 2,250 |
| | >10 | 1,330 | 2,080 | 2,210 | 2,250 |
| Viwanda | 0-10 | 1,240 | 2,080 | 2,210 | 2,250 |
| | >10 | 1,330 | 2,080 | 2,210 | 2,250 |
| Magati | | 500 | 1,740 | 1,850 | 1,880 |

**Jedwali Na. 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |
| Taasisi | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |
| Biashara | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |
| Viwanda | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |

**Jedwali Na. 3: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Inayopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

**Jedwali Na. 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Huduma ya Majitaka (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 400 | 650 | 700 | 750 |
| Taasisi | 650 | 850 | 950 | 1,000 |
| Biashara | 675 | 950 | 1,000 | 1,100 |
| Viwanda | 675 | 950 | 1,000 | 1,100 |

**Jedwali Na. 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Uondoaji wa Majitaka kwa Gari (Shilingi kwa Tripu)**

| Kundi la Wateja | Umbali (KM) | Tozo ya Sasa | Tozo Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Wateja Wote | 0-10 | 70,000 | 90,000 | 100,000 | 110,000 |
| | >10-20 | 80,000 | 100,000 | 110,000 | 120,000 |
| | >20 | 90,000 | 110,000 | 120,000 | 130,000 |

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea imeeleza kuwa bei zinazopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kuendana na ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo na hivyo kuhakikisha uendelevu wa huduma ya uhakika kwa wateja wake.

Tangazo hili limetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA Sura ya 414, kinachoitaka EWURA kutoa tangazo la taftishi ili kukusanya maoni kutoka kwa wadai ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (EWURA GCC), Baraza Ushauri la Watumiaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC), Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea na Umma kwa ujumla kuhusu bei zinazopendekezwa. Kama sehemu ya taftishi, kutakuwa na mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau utakaofanyika siku ya Jumatatu, tarehe 22 Agosti 2022 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kuanzia saa nne asubuhi.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 19 Agosti 2022. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea yanaweza kupatikana kwenye ofisi za Makao Makuu ya EWURA zinazopatika katika Jengo la EWURA, Medeli Magharibi, Dodoma au Ofisi za EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizopo Ghorofa ya Sita, Jengo la NHIF, Mtaa wa Karume, Mbeya Mjini au kwenye Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea zilizopo Songea Mjini.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**4 Agosti 2022**

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-3, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz

216987301

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# TANGAZO KWA UMMA

## MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MOSHI ("MOSHI WSSA") KWA MWAKA 2021/22 – 2023/24

Mnamo tarehe 11 Julai 2022, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Moshi (Moshi WSSA) la kutaka kurekebisha bei za huduma za majisafi na majitaka kwa mwaka 2022/23 hadi 2024/25. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

**Jedwali 1: Bei za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa (2021/22) | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | | | | |
| 0-10m$^3$ | 800 | 961 | 980 | 982 |
| >10<30m$^3$ | 940 | 1,129 | 1,152 | 1,154 |
| 30m$^3$ | 1,020 | 1,225 | 1,250 | 1,252 |
| Taasisi | 1,020 | 1,225 | 1,250 | 1,252 |
| Biashara | 1,150 | 1,382 | 1,409 | 1,412 |
| Viwandani | 1,250 | 1,502 | 1,531 | 1,535 |
| Magati | 800 | 961 | 980 | 982 |
| **Wastani wa Bei** | **997** | **1,198** | **1,221** | **1,224** |

**Jedwali 2: Bei Zinazopendekezwa za Kuondoa Majitaka kwa Mtandao (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 426 | 426 | 426 | 426 |
| Biashara | 418 | 418 | 418 | 418 |
| Biashara | 654 | 654 | 654 | 654 |
| Viwandani | 811 | 811 | 811 | 811 |
| **Wastani wa Bei** | **449** | **449** | **449** | **449** |

**Jedwali 3: Ada zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Makundi Yote ya Wateja | Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyoainiswa katika Kanuni ya 24 ya Kanuni za Maji 2013 | Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvukazi kama ilivyoainiswa katika Sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji 2013 | | |

**Jedwali 4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa rejesho)**

| Kundi la Wateja | Ada za sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwandani | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

**Jedwali 5: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Majitaka (Shilingi kwa tripu)**

| Kundi la Wateja | Ada za sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani (Ada za kumwaga) | 17,000 | 17,000 | 18,000 | 20,000 |

Kwa mujibu wa wasilisho la Mamlaka ya Maji Moshi, bei, ada na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kutekeleza kwa ufanisi shughuli za uendeshaji na uwekezaji kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2024/25. Mamlaka pia ilieleza kuwa kuidhinishwa kwa ushuru na ada zinazopendekezwa kutatekeleza shughuli zilizowekwa katika Mpango wa Biashara hivyo kuhakikisha uendelevu katika utoaji wa huduma za maji safi na maji taka kwa watumiaji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya Alhamisi, tarehe 25 Agosti 2022, katika ukumbi wa KILIMANJARO CRANE HOTEL, Moshi Mjini kuanzia saa 4:00 asubuhi kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe 1 Septemba 2022. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Ofisi za UWURA Kanda ya Kaskazini, GHOROFA YA PILI, JENGO LA PSSSF, KARIBU NA KIBO PALACE HOTEL, au Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi zilizopo mjini Moshi.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**
**03 Agosti 2022**

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-3, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz

21698730

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga SC, Simba iwe mechi ya kiwango, ufundi na ubora

**PAZIA** la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu mpya wa 2022/ 2023 linafunguliwa rasmi leo Agosti 13 kwa mchezo wa Ngao ya Jamii kati ya wenyeji Yanga dhidi ya Simba, ikiwa ni kiashirio cha kuanza rasmi kwa msimu.

Baada ya mchezo huu, wiki ijayo, Agosti 17, mwaka huu timu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo zitaanza mbio za kuwania taji hilo linaloshikiliwa na Yanga ya jijini Dar es Salaam.

Yanga ilitwaa ubingwa huo kwa kuwavua watani zao, Simba ambao walikuwa wanaushikilia kwa msimu wa nne mfululizo.

Mshindi wa taji hilo na timu inayoshika nafasi ya pili, zinapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Msimu uliopita, Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, raia wa Tunisia ilitwaa ubingwa huo kwa kuweka rekodi ya kutofungwa, lakini ikijihakikishia ubingwa ikiwa imebakiza mechi tatu mkononi.

Hata hivyo, kazi kwa Yanga haikuwa nyepesi, ilikutana na changamoto mbalimbali katika mbio hizo za kutimiza malengo yake.

Yanga ilipambana katika kila mechi, iliweka msimamo kwamba kila mchezo kwake ni fainali na kauli mbiu hiyo ilichangia kuongeza morari kwa wachezaji, viongozi, wanachama na mashabiki.

Hata hivyo, Yanga haikufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya CAF kwa kutolewa kwenye hatua za mapema wakati wapinzani wao, Simba wakiishia hatua ya robo fainali.

Baada ya maandalizi yao ya msimu mpya, sasa timu hizo zinakutana kwa mara ya kwanza msimu huu kwenye mchezo huu wa Ngao ya Jamii.

Kwa maandalizi yaliyofanywa na timu zote mbili ikiwemo mechi zao za kimataifa katika matamasha yao ya Siku ya Wananchi na Simba Day, Nipashe tunaamini kwamba, mchezo wa leo utakuwa wa kiwango cha juu na uliojaa ujuzi pamoja na ubora wa kimataifa.

Tunasema hivyo kwa sababu, timu zote mbili baada ya mechi zao za kujifua na zile za hivi karibuni za kimataifa dhidi ya Vipers ya Uganda na St. George ya Ethiopia, zimeona na kufanyia kazi mapungufu yaliyoonekana na benchi la ufundi.

Yanga kwenye kilele chao cha siku ya Wananchi ilipoteza kwa kufungwa mabao 2-0, wakati watani zao Simba waliibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Nipashe tunaamini kwamba, mabenchi ya ufundi ya Yanga na Simba yameona madhaifu ya timu zao na kila mmoja amejipanga vizuri zaidi kuelekea kuchezo huu wa leo utakaopigwa uwanja wa Benjamin Mkapa.

Nipashe hatutarajii kuona mchezo huo ukikosa ladha na burudani kwa wachezaji kucheza kwa shinikizo au mhemuko kutokana na ukubwa wa mchezo wenyewe, kwani huu ndio wakati wa kuonesha ubora wa vikosi vyao.

Na pia ni wakati wa wachezaji wapya kuonesha uwezo wao na kujiwekea imani kwa makocha wao kuwa na uhakika wa kupata nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

Zote Yanga na Simba zimefanya usajili mkubwa kwa kuimarisha na kuboresha vikosi vyao, hivyo leo sio siku ya majaribio bali ni siku ya kufanya kweli kwa wachezaji kuonesha ujuzi wao uwanjani.

Tunaamini kitakachooneshwa leo kwenye mchezo huu, ndio kitakuwa ufunguzi wa mechi nyingine nzuri zaidi katika mzunguko wa Ligi Kuu hadi kufikia mwisho wake.

Nipashe inazitakia Yanga na Simba mechi yenye kiwango, ufundi na ubora na tunaamini wachezaji pamoja na benchi la ufundi watalizingatia hilo ili mashabiki waweze kupata burudani nzuri na kuufurahia mchezo wenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Bila kiungo mkabaji, Simba ndoto kimataifa

Na Adam Fungamwango

**NI** ukweli usiopingika kuwa Simba ndiyo timu inayofanya vema zaidi kwenye michuano ya kimataifa hapa Tanzania, iwe Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Na wale siyo miaka ya hivi karibuni tu kama kizazi cha sasa cha soka la kwenye mitandao ya kijamii wanavyotaka kuaminisha watu, ila hata ukirejea historia ya soka la Tanzania, hadi leo klabu ambayo inaonyesha kuwa inafanya vema zaidi ni Simba.

Ndiyo timu ambayo mwaka 1974 iliwahi kufika hatua ya nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika ambayo kwa sasa inaitwa Ligi ya Mabingwa, lakini kama haitoshi iliwahi kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF) mwaka 1993.

Ukiachana na hapo ndiyo timu iliyotwaa hata Kombe la Kagame mara nyingi zaidi kuliko klabu yoyote ile Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Hata kuishia robo fainali ya Ligi ya Mabingwa siyo kama imefanya kwenye miaka ya hivi karibuni tu kama baadhi ya wanavyodhani, imefanya hivyo mwaka 1994, kabla ya kutolewa na Nkana Red Delvis ya Zambia.

Ni kwamba linapokuja suala ya michuano ya kimataifa kwa ngazi za klabu, Simba ndiyo imekuwa timu pekee inayoiheshimisha nchi, achilia mbali ushiriki wao wa miaka ya hivi karibuni uliochangia kwa kiasi kikubwa kupeleka timu nne kwenye michuano hiyo.

Kwa maana hiyo ni lazima ipewe ushauri pale ambapo tunaona kuna tatizo ambalo labda kocha mpya Zoran Maki hajalifahamu vizuri na Selemani Matola analifumbia macho kwa makusudi, kwa bahati mbaya au kutokujua, lakini pia viongozi wa Simba wanashindwa kuling'amua.

Ni kwamba baada ya kuteleza msimu uliopita, viongozi wa Simba na benchi la ufundi wamesajili wachezaji wa hadhi ya juu kwa gharama kubwa, pia wenye uwezo mkubwa ambao umethibitishwa kwenye mechi dhidi ya St George Agosti 8 mwaka huu. Simba ilishinda mabao 2-0 na baadhi ya mapungufu ya msimu uliopita yakaonekana kutatulika.

Kwa sasa timu ina viungo washambuliaji wengi wazuri, wabunifu na mawinga hatari kama ni Agustine Okra, Nelson Okwa, wakiunganika na kina Clatous Chama, Pape Sakho, Peter Banda, wakiungana na straika Moses Phiri na wengineo.

Tumemuona beki wa kati Mohamed Ouattara alivyoituliza beki kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, Simba bado inaendelea kukosa kiungo mkabaji katili pale katikati mwenye nguvu, mapafu ya mbwa na kugongana na wachezaji wa timu pinzani, kuwapora mipira, kunusa hatari, ambaye kazi yake kubwa anayoifanya na kuipenda ni kuzuia zaidi kuliko kushambulia.

Wengine wanawaita wachezaji wa kazi chafu. Huyo ndiye mchezaji anayekosekana kwa upande wa Simba.

Mabeki wa Simba wanafikiwa kwa urahisi zaidi na wapinzani wao kwa sababu viungo wote wakabaji wa Simba waliopo, ni wale ambao wako vizuri wanapokuwa na mpira miguuni na si wakati hawana mpira.

Ni wavivu wa kukaba, kufuata wapinzani wanapokuwa na mpira, wana tabia ya kutegeana na waoga pia kuingiza miguu mpinzani anapokuwa na mpira.

Ukiwa una kasoro kama hizo, basi huwezi kuwa kiungo mkabaji mzuri na itakuwa ni hasara tu kwa timu yako.

Nimeshangaa pamoja na usajili wote bado haikusajili kiungo mkabaji, sehemu ambayo ni muhimu mno kwenye soka kwani unaweza ukapata bao moja tu, ukafunga duka.

Ukiangalia hata timu kubwa kama Al Ahly, wanaweza kusajili wachezaji wazuri sana, lakini huwa wana viungo wao wakabaji ambao mara nyingi ni vipande vya watu kutoka Afrika Magharibi. Kazi yao hao ni kufanya uchafuzi tu pale kati. Sina wasiwasi sana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, kama Simba inakwenda na viungo wakabaji hawa waliopo, basi inaweza kutolewa mapema kwenye michuano hiyo na mashabiki wakaanza kupiga kelele kuwa usajili mbovu.

Kumbe haina watu kama Gerson Fraga, au Thadeo Lwanga yule wa mwanzo wakati anawasili. Miaka ya nyuma ilikuwa na kina Abbas Kuka, Ramadhani Lenny, Idd Selemani 'nyigu' aliyefariki wiki hii na kuzikwa Manzese, Nico Nyagawa, Matola mwenyewe na wengineo.

Naamini Simba ikimpata kiungo mwenye akili ya kuzuia zaidi hata kama Zawadi Mauya tu, wala siyo Yannick Bangala mwenye uwezo mkubwa zaidi, basi inaweza kufika mbali.

Kwa hawa waliopo kina Jonas Mkude, Mzamiru Yassin, Sadio Kanoute, ama Victor Akpan ambaye naye si mkabaji halisi, bali ni namba nane, Simba itahenyeka sana kimataifa, hasa ikikutana na timu zenye kasi na zinazoshambulia mfululizo.

**HABARI KITAIFA**

# Mahakama yaibana Jamhuri upelelezi wa kesi ya Sabaya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Moshi, imeuweka kikaongoni upande wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wanne, kuutaka kukamilisha upelelezi kwa wakati.

Aidha, mahakama hiyo imeshangazwa na upande huo kushikilia hoja ya kutokamilika kwa upelelezi huku ikijua washtakiwa hao katika kesi namba 2 ya mwaka 2022 wanateseka gerezani.

Akijibu hoja za upande wa utetezi, Hakimu Mkazi Mfawidhi, Salome Mshasha, alisema mahakama iko kwa ajili ya kutoa haki na si kunyanyasa upande wowote huku akikiri washtakiwa hao kukaa takribani miezi miwili gerezani bila kujua hatima yao.

"Mahakama iko kwa ajili ya kutoa haki na siyo kunyanyasa upande wowote, ni vyema upande wa Jamhuri ukamilishe upelelezi pamoja na kibali ili washtakiwa wajue haki zao," alisema.

Hakimu alieleza kushangazwa kwake kwamba tangu kesi imepelekwa mahakamani hapo upande wa Jamhuri umekuwa ukitoa sababu za kutokamilika kwa upelelezi.

Sababu nyingine ni pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwamba haijatoa kibali kwa mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu alisema mahakama haiwezi kuvumilia upande wa Jamhuri kutoa sababu za aina moja kila wakati licha ya washtakiwa kuendelea kuteseka bila kujua hatima yao.

"Nimesikiliza upande wa utetezi na nimebaini wana hoja. Hatuwezi kuendeleza kuvumilia hili na huu ni muda wa kwenda msikitini. Naahirisha shauri hadi Agosti 29, 2022 tutakapokuja kujibu vifungu vya sheria vinavyoainishwa na upande wa utetezi," alisema.

Akiwasilisha hoja, Wakili wa Jamhuri, Sabitina Mcharo, aliiomba mahakama kuahirisha shauri hilo kwa madai upelelezi haujakamilika pamoja na kutopatikana kwa kibali cha mahakama kuisikiliza kesi hiyo.

"Zipo hoja zinazotolewa na upande wa utetezi. Tumezisikia na tutaziwasilisha kwa viongozi wetu kwa ajili ya utekelezaji," alidai.

Awali, akiwasilisha hoja za utetezi, Wakili Moses Mahuna alidai kuwa sasa ni mwaka mmoja na miezi sita tangu washtakiwa kudaiwa kutenda kosa hilo.

"Washtakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo Februari 22, 2021 na hadi leo ni mwaka na miezi sita na walifikishwa mahakamani Juni 1, mwaka huu. Tunaamini Kwamba upelelezi ulitakiwa kuwa umekamilika lakini bado ni kinyume chake," alidai.

Wakati shauri hilo linafunguliwa, alidai kuwa walielezwa kwamba upelelezi umekamilika lakini baadaye hoja zikabadilika na kudai haujakamilika, hivyo ni ombi la utetezi washtakiwa waachiwe hadi upelelezi ukamilike.

"Tangu kesi ifunguliwe Juni mosi hadi leo (jana) ni miezi miwili imepita. Nini kinasababisha upelelezi usikamilike? Mahakama itazame kifungu cha 62 cha tafsiri ya sheria, kuwa endapo sheria haijatoa ukomo wa jambo kufanyika, jambo hilo linapaswa kufanyika kwa sababu za uzoefu," alidai Mahuna.

Wakili Mahuna alihoji kama upelelezi haujakamilika kwanini washtakiwa hao walikamatwa, hivyo kuiomba mahakama imlazimishe DPP akamilishe upelelezi.

Pia aliomba washtakiwa waachiwe na warejeshwe mahakamani mara upelelezi utakapokamilika. Mahakama iliahidi kujibu hoja hizo Agosti 29, kesi hiyo itakapotajwa.

## CCM: Uchaguzi utarudiwa tukibaini wamepanga safu

**Na Mary Geofrey,** MUHEZA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema atafuta uchaguzi wa ndani wa chama kwa maeneo ambako itabainika kuna wanachama waliopanga safu ya uongozi kwa maslahi binafsi.

Chongolo pia ameonyesha kuchukizwa na mgogoro wa viongozi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, unaosababisha kuchelewesha miradi ya maendeleo.

Mtendaji huyo wa chama alibainsiha hayo juzi wilayani humo alipozungumza kwenye mkutano wa wanachama na watendaji wa serikali, akiwa kwenye ziara yake ya kukagua ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhimiza sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23 mwaka huu.

Alisema chama hicho ni kikubwa na hakiwezi kufanya mambo yake kienyeji ya kuchagua viongozi kwa njia na taratibu zisizo sahihi.

Alimtaka Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Saimon Renyesa, kusimamia mambo anayotakiwa kufanya kwa mujibu wa taratibu za chama.

CCM inaendelea na uchaguzi ndani ya chama ngazi ya matawi, kata, wilaya na mkoa kwa jumuiya zote.

Kuhusu mgogoro wa viongozi wilayani Muheza, Chongolo alitoa miezi mitatu kwa viongozi hao kukaa na kumaliza tofauti zao ili kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Wale wenye dhamana na wilaya hii kaeni, Halima (Bulembo - Mkuu wa Wilaya) wewe ndiyo unajua jahazi la hapa, wewe ndiyo mwakilishi wa Rais Samia hapa, kaa na wenzako, mtu akiwa haendi kwenye mstari, mpeleke kwenye mstari kwa lazima, toa taarifa, sema, usiogope hata ukiwa mfupi hivi (akionyesha saizi ya chini) uwe na umri mdogo aliyekuamini anajua unaweza kuitendea haki hiyo nafasi," aliagiza.

Alieleza zaidi kuwa, alipokuwa Wilaya ya Lushoto, aliona ushirikiano kila mtu anafahamu anachotakiwa kufanya, akisisitiza 'hapa hakuna!'

"Mkurugenzi umeletwa hapa kusimamia halmashauri, kama kuna mtu aliye mrefu kuliko wewe, ni huyo RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) hapo ndiyo kiongozi wako, kiongozi wako ni huyo mkuu wa wilaya lazima mjue hivyo," alielekeza.

Alimtaka Katibu Mkuu wa Mkoa, Pili Mnyema, kusimamia kanuni na taratibu za mkoa huo ili kumaliza dosari hiyo.

Aliahidi kuwa jambo hilo halitafumbia macho na atalifikisha kwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa uzito unaostahili ili kuwasaidia wananchi wa Muheza.


TUSAIDIANE PASADA

216988701

# TANGAZO LA ZABUNI

ACHIEVE ni mradi wa miaka mitano (2020-2024) unaotekelezwa katika nchi tisa duniani. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).

Kwa Tanzania, ACHIEVE ni mradi wa miaka minne (2020-2024) unaolenga katika kuboresha huduma za kukabiliana na Virusi vya UKIMWI (VVU) miongoni mwa watoto waishio katika mazingira hatarishi. Kufikia lengo hili, Mradi wa ACHIEVE unatoa huduma kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi na kutekeleza afua ya DREAMS. Pia, Mradi wa ACHIEVE umelenga kuboresha mifumo ya huduma za ustawi wa jamii ili kuboresha ubora na upatikanaji wa huduma hizo. Vilevile, Mradi wa ACHIEVE unajengea uwezo na kuzisaidia AZAKI za wazawa kuwa na mifumo rasmi na imara ya kiutendaji kwa ajili ya huduma endelevu katika ngazi ya jamii. Mradi wa ACHIEVE unatekelezwa katika Halmashauri 95 zilizopo katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mradi wa ACHIEVE unatekelezwa na Shirika la Pact kama Shirika Kiongozi kwa ubia na mashirika ya Palladium, No Means No, na WI-HER. Wabia hawa wanatekeleza mradi wa kusaidiana na AZAKI za wazawa ikiwemo PASADA

Pastoral Activities and Services for People with AIDS Dar- es- Salaam Archdiocese (PASADA) ni taasisi ya dini chini ya Kanisa Katoliki jimbo la Dar es Salaam yenye makao yake makuu Dar es Salaam. PASADA inatekeleza miradi mbalimbali katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

USAID ACHIEVE project ni moja kati ya Miradi inayotekelezwa na PASADA katika mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kwa lengo la kujengea uwezo jamii ili kuiwezesha kutatua changamoto zao na kuboresha maisha yao, kuwa na afya njema na kunufaika na rasilimali zilizopo.

PASADA inatangaza zabuni toka kwa watu binafsi, makampuni kutuma maombi ya zabuni ya upatikanaji wa sare za wanafunzi 3035 wa kike/kiume zenye sifa zifuatazo :

| Na | Bidhaa | Maelezo | Kiasi/Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Sare ya Shule za Msingi | Shati | 3035 |
| | | Kaptula / Sketi | 3035 |
| | | Jozi ya Soksi | 6070 |
| | | Sweta | 3035 |

***Maelekezo:*** *Fomu hii inaelezea sifa za sare kwa wanafunzi wa shule za msingi wa kike/ kiume ambao ni wanufaika wa mradi wa ACHIEVE, unaofadhiliwa na watu wa Marekani (USAID).*

**Sifa za Sare za shule**

| Na | Bidhaa | Sifa |
|---|---|---|
| 1 | Shati | Shati jeupe (Tomato) lenye mfuko mmoja upande wa kushoto |
| 2 | Sketi | Sketi za watoto wa kike kulingana na rangi za shule husika. |
| 3 | Kaptula | Kaptula za watoto wa kiume kulingana na rangi za shule husika |
| 4 | Soksi | Soksi kulingana na rangi za shule husika |
| 5 | Sweta | Lililofumwa kwa nyuzi kulingana na rangi za shule husika. |

*Mzabuni anatakiwa aombe zabuni ya kushona/kuuza sare za shule kwa ajili ya watoto kuanzia 300 (ambazo itakuwa na sketi (moja) au Kaptula (moja)-, Shati (moja-aina ya Tomato), soksi (jozi 2) na Sweta la shule (moja).

**Mzabuni anatakiwa awe na vitu vifuatavyo:**
- Awe na mashine ya kutolea risiti ya kielektroniki (EFD).
- Uwezo wa kukabidhi sare kama mkataba unavyoonesha pasipo kupewa malipo ya awali (No advance payment).

Wazabuni watakaotuma maombi wanatakiwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

1) Nakala ya leseni ya biashara,
2) Nakala ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN)
3) Nakala ya Cheti cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT)
4) Nakala ya uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax Clearance)
5) Muda atakaotumia kukamilisha kazi.
6) Taarifa na viambatanisho vinavyoonesha ameshawahi kufanya kazi kama hii na taasisi nyingine (Purchase Order)
7) Wasifu wa kampuni/taasisi (Company profile)
8) Taarifa ya ukaguzi wa fedha ya mwaka uliopita (Audited financial report)
9) Sampuli ya bidhaa kama ifuatavyo

- Kitambaa cha kaptula / Sketi cha rangi ya bluu iliyoiva (Dark Blue) aina ya ESEEM No. 1 India
- Shati aina ya Tomato (Pure Cotton No. 1)
- Soksi Nyeupe

Wazabuni wenye sifa/vigezo wawasilishe maombi yao kwa mkono kupitia anuani ifuatayo:

**KAMATI YA ZABUNI**
**PASADA**
**Chang'ombe, Temeke**
**S.L.P 70225**
**Dar Es Salaam.**

***Ofisi zipo ndani ya eneo la Kanisa Katoliki Parokia ya Mt. Fransisko Xavery Chang'ombe (Mkabala na Kituo cha Polisi – Chang'ombe) Temeke.***

Maombi yote yawasilishwe katika bahasha iliyofungwa lakiri (Seal). Mwisho wa kupokea maombi ni;

**Tarehe: 22/08/2022**
**Muda: Saa 5:00 Asubuhi.**

**Tafadhali Zingatia:**
1. Maombi kwa njia ya barua pepe au simu hayatapokelewa.
2. PASADA wanaweza kukataa ombi lolote au maombi yote yaliyopokelewa kwa sababu maalum.
3. PASADA ina haki ya kuyakataa maombi yoyote yatakayowasilishwa na mzabuni endapo mzabuni atashindwa kufuata taratibu zilizowekwa.
4. Malipo yatafanyika baada ya mzabuni kukabidhi sare za shule na PASADA kujiridhisha.
5. Zabuni itafunguliwa tarehe 22/08/2022, saa 5 :30 Asubuhi katika ofisi za PASADA – Chang'ombe, Temeke – Dar es Salaam.

## RC awa mbogo kuhusu mashamba pori

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

SERIKALI mkoani Singida imesema itawanyang'anya na kuyagawa kwa wengine wakulima waliopewa mashamba katika skimu ya umwagiliaji Itagata, Itigi wilayani Manyoni ambao wametelekeza ekari 169 bila kuziendeleza.

Msimamo huo ulitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, baada ya kuitembelea skimu hiyo ambayo serikali ilitumia zaidi ya Sh. bilioni 2.1 kujenga lakini idadi kubwa ya wakulima hawalimi huku wengine wakiyakodisha kwa watu wengine.

Alisema, serikali haiwezi kukubali kuona katika mradi huo ambao iliekeza mabilioni ya fedha, ekari 40 tu ndizo zonazolimwa kati 209 walizogawiwa wakulima ambao ni wananchama wa Umoja wa Umwagiliaji Itigi.

"Serikali imewekeza fedha nyingi sana kwenye mradi huu lakini hatujautendea haki na hata maji yakifika hapalimwi. Hii haikubaliki lazima watu walime ili kuisaidia serikali kupata mapato na Tume ya Umwagiliaji nao wapate tozo zao," alisema.

Serukama alisema, matumaini ya serikali ni kuona eneo lote linalimwa wakati wa kiangazi na masika ili baada ya hapo ijengwe hoja ya kutaka kuongezewa eneo lingine la kulima.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa alimwagiza Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Diwani na Mtendaji Kata kuandaa mkutano kuzungumza ili wawe wenye uwezo wa kulima wasikodishe mashamba badala yake wapewe wengine wenye uwezo wa kulima.

"Mwezi wa tisa mwenyekiti andaa mkutano na wanachama wako ili tuje tujue nani analima na nani halimi ili wale ambao hawalimi tuwaondolee mashamba tuwape wengine ambao watalima na kuipatia Serikali mapato pamoja na Tume ya umwagiliaji," alisema.

Serukamba alisema, wakulima lazima watambue kuwa faida atakayoipata mkulima kupitia kilimo kwenye skimu hiyo itamrahishia maisha kiuchumi ataweza kuhudumia familia, kulipa bima ya afya pamoja na kuchangia maendeleo ya taifa lake.

"Kuna watu kule Dodoma hawana maji na wangetamani kulima lakini nyie mmepata bahati ya maji lakini hamtaki kulima hatueleweki unayetaka kulima vitunguu, mahindi mpunga lima," alisema.

Serukamba alisema, serikali imetoa mbolea ya ruzuku ambayo sasa itakuwa inauzwa Sh.70,000 hivyo wakulima wajifunze na matumizi ya mbolea katika kilimo hicho.

Mmoja wa wakulima katika skimu hiyo, Chacha Marwa alisema changamoto inayokabili wakulima wengi kutolima ni kushindwa kutambua aina ya udongo pamoja na baadhi ya wanachama wa umoja huo wa umwagiliaji waliopewa mashamba kuyakodisha kwa watu wengine.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, sisi huu udongo unatuchanganya sana tunashindwa kuelewa tulime mbegu gani tunaomba mtusaidie kutupimia udongo wetu," alisema.

Chacha alisema, kuwa baadhi ya wasimamizi wa skimu hiyo sio waaminifu kwa wanachama wao jambo linalopelekea washindwe kufanya shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwani wamekuwa wakikodisha mashamba na kuwanyima fursa wengine.

Awali, Mwenyekiti wa Umoja wa Umwagiliaji Itagata, Stephen Mbonge, alisema mashamba yenye ukubwa wa ekari 209 yaligawiwa kwa wanachama 321 ambapo ekari 106 ziligawiwa kipindi cha masika.

# NHC yavuta wawekezaji kutoka 'Sauzi'

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limesema litahakikisha linatatua migogoro katika maeneo ya makazi na biashara kwa kuendelea kujenga majengo yatakayopangishwa au kuuzwa kwa gharama nafuu kulingana na hali ya mwananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Nehemia Mchechu, alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao na Chama cha Wafanyabiashara wa Afrika Kusini chenye lengo la kuwashirikisha kufahamu fursa zilizopo ndani ya shirika hilo.

"Tunakwenda kujenga nyumba aina ya magorofa nchi nzima ili kujibu matatizo ya maeneo ya biashara na makazi ya watu ambayo tutauza na kupangisha kwa gharama nafuu kwa kufuata taratibu zilizowekwa," alisema.

Mchechu alisema NHC ina mpango wa kuwa na miradi katika viwanja vya Kawe, Magomeni Mchikichini, Temeke Mwisho, Magomeni na Kinondoni, akisisitiza maeneo hayo kwa asili yalikuwa mali ya shirika hilo, hivyo yakirejeshwa kwao, ujenzi utaanza mara moja.

Alisema wanaendelea kumaliza miradi ya kimkakati ambayo ilikwama na sasa wataitangaza kwa wawekezaji wakubwa kutoka nchi jirani ambazo zina uwezo wa kuwekeza nchini.

"Tunaamini wawekezaji ni muhimu sana na sisi tunatembea katika mapito ya The Royal Tour kwa kutangaza fursa na kuwaleta wawekezaji na NHC tuna mikakati mipya, sasa hivi tumepanga kwa kushirikiana na sekta binafsi," alisema Mwenyekiti wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini, Manish Thakrar, alisema NHC wamewaonyesha fursa nyingi za kuja kuwekeza na siyo kwao pekee, bali pia mataifa mengine.




Meneja wa Bidhaa wa kampuni ya LG Afrika Mashariki, Eden Seo (kushoto), akiwa na Mkuu wa LG Afrika Mashariki, Sa Nyoung Kim (katikati) na Mkurugenzi Mkuu wa Opalnet, Rakesh Singh, wakati wa uzinduzi wa friji mpya za LG, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SBL yaendesha mafunzo kwa vitendo wanasayansi wanawake

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imechukua vijana wa kike 10 wanaofanya vizuri katika fani za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM) waliohitimu katika vyuo mbalimbali na kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo katika viwanda vyake.

MKURUGENZI wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam kuhusu mchango wa kampuni hiyo katika kuongeza ushiriki wa vijana wa kike katika fani ya sayansi na teknolojia nchini.

Alisema tangu kuanzishwa kwa program ya STEM mwaka jana, tayari vijana 20 wamenufaika na mpango huo kwa kupata fursa ya kujifunza kwa vitendo kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye viwanda vyake vilivyoko Moshi, Mwanza na Dar es Salaam.

"SBL imechukua vijana wengine 10 wa kike katika programu hii kwa mwaka huu, baada ya mwaka jana kuchukua idadi kama hiyo. Jumla ya vijana wa kike 20 wameshanufaika na programu hii na programu hii ni endelevu na inalenga kuongeza ushiriki wa vijana wa kike katika fani za sayansi na teknolojia.," alisema Wanyancha.

Aliongeza kuwa programu ya STEM ilianzishwa mwaka jana ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali na kusaidia ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi hususani kupitia fani za sayansi na teknolojia ambazo zina mchango mkubwa katika kuleta maendekeo ya haraka kwa taifa.

Sambamba na hilo, alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 STEM imetambua teknolojia mpya 90 zilizozalishwa nchini, hivyo kufanya teknolojia zilizotambuliwa hadi sasa kufikia 479 kwa lengo la kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na bunifu nchini.

"SBL kama mwekezaji na mmoja wa waajiri muhimu nchini, inatumia program hiyo ya STEM kuhakikisha usawa wa kijinsia unadumishwa katika nyanja mbalimbali ndani ya kampuni hiyo na kusambaa kwa jamii kwa ujumla," alisema Wanyancha

Glory Hungu, mmoja wa wanufaika wa STEM kutoka SBL, alithibitisha program hiyo ilivyo na manufaa akisema imemvutia kwa vile imejikita katika masomo sayansi, teknolojia, uhandisi na hesabu na kuhamasisha ubobezi kwa wanawake.

"Tangu nimepata nafasi ya kujiunga na program hii, nimejifunza mambo mengi katika kuwa na fikra pevu, uwazi na kunipa uzoefu wa kazi. Ninategemea kujifunza mengi na kutanua uelewa wangu katika uongozi na ujuzi wa kazi, pia kukuza kipaji changu kupitia program hii" alisema.



# RC asema yuko tayari kukosolewa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema yuko tayari kukoselewa wakati wowote katika utendaji kazi wake wa kuwahudumia wananchi.

Senyamule aliyasema hayo, jana alipokuwa akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kujitambulisha kwao baada ya kuhamishiwa Dodoma akitokea mkoa wa Geita.

Alisema yeye yupo tayari kukosolewa wakati wowote na viongozi wa CCM katika utendaji wake wa kuwahudumia wananchi kwa sababu anatekeleza ilani ya chama hicho. "Mimi ni mgeni naomba katika mkoa huu mkiona naenda ndivyo sivyo kwenye utendaji wangu, nikosolewe ili tuwahudumie wananchi wa mkoa wetu," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alisema, anaujua uongozi wa CCM Mkoa una vipaumbele ambavyo vimewekwa katika kuwaendeleza wananchi kiuchumi, hivyo atakuwa tayari kushirikiana nao.

Aidha, Senyamule alisema atafanya ziara katika wilaya zote kuangalia hali ya uchumi katika kila eneo ili kuwasaidia wananchi. Alibanisha kuwa vipaumbele vyake katika utendaji kazi wake mkoani hapa ni kilimo, elimu, na mambo ya mazingira kwa ujumla.

Kuhusu mazingira, alisema ataendeleza kampeni ya kufanya Dodoma kuwa ya kijani na atashirikiana na viongozi wengine wa mkoa na kitaifa katika kutimiza azma hiyo.

Aidha, kuhusu kilimo, alisema anatarajia kuwahamasisha wananchi kutumia fursa ya ukame uliopo hapa ili kuinua hali ya uchumi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, alimtaka kiongozi huyo kushirikiana nao ili kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2025.



Wazari wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akipanda mti wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji wa miti katika Kata ya Ipagala, Jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wakulima wahimizwa kutumia teknolojia kuzalisha kwa tija na kuinuka kiuchumi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHUO cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimewataka wakulima kutumia kilimo cha kiteknolojia ili kusaidia kuchochea mnyororo wa thamani katika mazao wanayolima.

Akizungumza jana na Nipashe, Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Chuo hicho, Godrick Ngoli, alisema hivi sasa dunia imebadilika, hivyo wakulima nao wanapaswa kukifanya kilimo chao kuwa cha kibiashara.

Kwa kufanya hivyo, alisema kutawasaidia kuinuka kiuchumi pia kuongeza mnyonyoro wa thamani ya mazao

"Wakulima mnapaswa kubadilika kwenye suala zima la kilimo, hasa ukizingatia serikali imewekeza bajeti kubwa kwenye kilimo. Tumieni fursa hiyo kupanua wigo wa kilimo mnachofanya," alisema Ngoli.

Alisema chuo cha mipango kina wataalamu mbalimbali ambao wanatoa elimu kwa jamii ya namna ya kuendesha na kushauri katika masuala mbalimbali ya uzalishaji kadhaa zikiwamo za kilimo, mifugo na uvuvi.

Ofisa Mipango wa Chuo hicho, Francis Mbonde, aliwahamashisha wananchi kujiandaa na kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarijiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Alisema jambo hilo ni muhimu kwa sababu serikali ina nia njema ya kutaka kujua idadi ya watu pamoja na makundi mbalimbali, mahitaji yao katika kuendesha shughuli zao na taifa kwa ujumla.

# Kikwazo mitaala ustawi chatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KUTOKUWAPO ubora wa mafunzo ya ustawi wa jamii ni kuiga baadhi ya kozi za kada ya afya bila kujali mahitaji ya mitaala, imeelezwa.

Kutokana na hali hiyo, serikali imevitaka vyuo binafsi vya taaluma ya Ustawi wa Jamii kwa ngazi ya astashahada na stashahada nchini kushirikiana ili kuhakikisha kunakuwa na mitaala linganifu ya uendeshaji wa mafunzo hayo ili kuwa na wataalamu wenye umahiri na viwango vinavyohitajika.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Patrick Golwike, alisema hayo jana kwenye kikao kazi kati ya wizara na wakuu hao.

Golwike alisema, ili kutatua kero hizo, wizara ilitengeneza mitaala linganifu ya kitaifa pamoja na nyenzo zake za kufundishia kozi ya ustawi wa jamii ngazi ya astashahada na stashahada kwa nchi nzima.

"Eneo pekee lililokuwa limebaki ni kuanzishwa kwa mfumo wa mitihani ya pamoja ili kutahini wanafunzi kwa ubora na viwango sawa. Kuna vyuo vinaendesha mafunzo ya kozi hiyo kwa kuiga uzoefu wa mfumo wa kozi za afya kwa baadhi ya maeneo bila kujali mahitaji ya mitaala na utofauti wa kada ya ustawi wa jamii na kada ya afya," alisema.

Pia alisema, baadhi ya vyuo kutokuwa na wakufunzi wa kutosha, kuendesha mafunzo kwa kutumia walimu ambao hawana sifa za kufundisha kozi ya ustawi wa jamii kama vile wauguzi, maendeleo ya jamii, walimu wa sekondari kinyume na matakwa ya mitaala pamoja na kutunga mitihani ambayo haina viwango vya kupima weledi na umahiri wa wahitimu.

"Hali hii imeathiri kwa kiwango kikubwa ubora wa mafunzo ya ustawi wa jamii na kutoa rasilimali watu isiyokuwa na weledi na maarifa stahiki hivyo, tukiweka utaratibu mzuri tutamaliza changamoto hizi na kuwa na vyuo vinavyotoa wataalamu mahiri," alisema Golwike. Awali, Mwakilishi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii wa Wizara hiyo, Lomito Mollel, alisema lengo la kikao kazi hicho ni kujadili namna ya kusaidia uboreshaji wa mitaala ili kuhakikisha taaluma ya ustawi wa jamii itatoa wataalamu mahiri na bora.

Mmoja wa Wakuu wa Vyuo kutoka Chuo cha Afya cha Eliseray kilichopo mkoani Tanga, Charles Mselema, alisema vyuo hivyo vitaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha vinatoa wataalamu mahiri na bora wa ustawi wa jamii ili kusaidia kutatua kero mbalimbali ikiwamo upungufu wa wataalamu hao.





# TMA yatakiwa kutangaza shughuli zake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetakiwa kutangaza ili taarifa zao zisikike kwa jamii, hatua ambayo itasaidia kuleta maendeleo katika makundi mbalimbali yakiwamo ya wakulima ili kuwawezesha kuendesha shughuli zao.

Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Suleiman Masoud Makame, alisema hayo juzi alipotembelea banda la mamlaka hiyo katika Maonyesho ya Kilimo, yanayoendelea Kizimbani, mjini Unguja.

Alisema, taarifa zinazotolewa na TMA ni muhimu na zinatakiwa ziwafikie walengwa wakiwamo wakulima.

Waziri alisema, wananchi bado hawana uelewa wa kufuatilia taarifa zinazotolewa na mamlaka hiyo, kwa upande wa Zanzibar tofauti na nchi zingine ambazo wananchi hawawezi kufanya shughuli zao bila kupata taarifa za taasisi hiyo.

Alisema, wavuvi wanahitaji kupata taarifa sahihi za hali ya hewa kabla ya kuanza shughuli zao baharini ili kuepuka matukio yanayojitokeza mara kwa mara hususan ajali zinazotokana na kuchafuka kwa hali ya hewa baharini.

"Taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa wavuvi ni muhimu kabla ya kuanza shughuli zao ili kukabiliana na matukio ya ajali zinazosababishwa na kuchafuka kwa hali ya hewa ikiwamo upepo mkali," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Hali ya Hewa Zanzibar, Masoud Makame, alisema wamejipanga kuhakikisha taarifa zinazotolewa na mamlaka hiyo zinawafikia wananchi wote. Alisema, hivi sasa wanatoa taarifa zao kupitia vyombo vya habari katika vipindi tofauti na kuwataka wananchi ikiwemo makundi maalumu, wavuvi, na wakulima kuziamini hizo.

Pia alisema mamlaka hiyo imejipanga kufanya kazi kitaalamu zaidi baada ya kupata vifaa vya kisasa vya teknolojia ya mawasiliano hatua ambayo imewezesha kutekeleza majukumu vizuri na kuaminika.

"Wito wangu wananchi na makundi mengine kuziamini taarifa zetu za hali ya hewa. Tumejipanga zaidi kuyafikia makundi yote ili taarifa zetu wazitumie kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo yao," alisema.

Baadhi ya wananchi waliofika katika banda la Mamlaka ya Hali ya Hewa Zanzibar waliitaka taasisi hiyo kufikisha taarifa zake zaidi kwa kutumia vyombo vya habari vikiwamo vya binafsi ili ziwafikie watu wengi na kujipanga kwa matukio yanayoweza kujitokeza.




Mshindi wa gari la nne kupitia shindano la Vodacom Tusua mapene, Editha John mkazi wa Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, akifungua mlango wa gari lake jipya aina ya Suzuki S Presso, baada ya kukabidhiwa katika viwanja vya stendi ya zamani Iringa mjini. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo na Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ezekiel Nungwi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yapewa kibarua kizito uwajibikaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi limetakiwa kuongeza kasi ya uwajibikaji ikiwamo nidhamu pamoja na kufuatilia kwa karibu matukio mbalimbali ya uhalifu yakiwamo ya udhalilishaji wa kijinsia ili kujenga heshima na hadhi kwa wananchi.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, alipofanya mazungumzo na Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis, aliyefika ofisini kwake, Vuga kujitambulisha baada ya kuteuliwa hivi karibuni. Hemed alisema, Jeshi la Polisi limekabidhiwa majukumu makubwa ambayo ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kudhibiti matukio ya uhalifu yanayotishia maisha ya wananchi.

Alisema, miongoni mwa matukio ambayo yamekuwa yakizusha maneno na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ni juu ya ushughulikiaji wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia na mwenendo wake hadi zinapofikishwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Hemed, bado baadhi ya kesi zinachukua muda mrefu kukamilika kwa upande wa upelelezi kiasi cha wananchi kukata tamaa na wengine kushindwa kufika mahakamani kutoa ushahidi.

"Ziko changamoto za Jeshi la Polisi kuchelewa kukamilisha upelelezi wa kesi kwa ajili ya kufikishwa mahakamani. Hili tunataka mlifanyiye kazi haraka kesi zisichukue muda mrefu," alisema. Hemed pia alilitaka jeshi hilo kuongeza ushirikiano na kufanya kazi kwa pamoja na idara maalumu ya vikosi vya serikali ya Zanzibar katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao unadumishwa.

Naye Kamishna Hamad alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha changamoto zote ambazo ni kero kwa wananchi zinapatiwa ufumbuzi hatua ambayo itasaidia kuleta ufanisi ndani ya jeshi hilo.

Alisema majukumu ya Jeshi la Polisi yapo wazi ambayo ni kulinda usalama wa raia na mali zao pamoja na wageni, hivyo wamejipanga kuona usalama wa wageni wakiwamo watalii, unaimarishwa kwa kushirikiana na kikosi cha polisi utalii. Sekta ya utalii, alisema ni tegemeo la taifa, hivyo ulinzi wa wageni katika maeneo ya fukwe za mkoa wa Kaskazini Unguja na Kusini utaimarishwa ili Zanzibar iendelee kuwa kisiwa salama kwa wageni.

# Mwinyi apania kuinua vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itahakikisha inapanga mipango yake ya maendeleo na ukuaji wa uchumi kwa kuwashirikisha vijana na kufikia malengo yao ya kujiajiri.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdull wakati wa maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani.

Alisema serikali itahakikisha inatoa vipaumbele kwa kundi la vijana katika kuwapatia mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi ili kuendelea na masomo yao.

Katika kuhakikisha vijana wanapiga hatua kubwa ya maendeleo, alisema serikali yake imetenga fedha nyingi kwa ajili ya wajasirimali vijana ili kupiga hatua kubwa ya kiuchumi na maendeleo.

Alisema hayo ndiyo malengo ya serikali ya Zanzibar kuhakikisha kwamba vijana wanafikia malengo ya kujaijiri na kuondokana na utegemezi wa ajira serikalini.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tutahakikisha mipango yetu yote ikiwamo ya bajeti na kimkakati inawahusisha vijana kwa ajili ya kuleta mabadiliko na mageuzi makubwa," alisema.

Dk. Mwinyi aliwataka vijana kujiunga katika mabaraza ya vijana ambayo yameanzishwa ikiwa ni chemchemu ya fikra mpya za kuleta mabadiliko ya kujenga nchi.

Pia aliwahimiza vijana kuendelea kuunga mkono juhudi na mipango inayopangwa kutekelezwa na serikali na kushirikiana katika kuhakikisha wanaitekeleza ilani ya CCM kwa mafanikio makubwa.

Aidha, aliwataka kutumia fursa wanazoandaliwa na serikali, kushirikiana pamoja na kufanya kazi kwa bidii huku wakiwa wamejiwekea malengo ya muda mfupi na muda mrefu katika maisha yao.



## ABDUL KIBA

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT

JUMAMOSI AGOSTI 13, 2022



# KIZZ DANIEL

# Nani wa kumpa pole?

WIKI hii tasnia ya burudani nchini ilikumbwa na taharuki baada ya mwanamuziki kutoka Nigeria, Kizz Daniel, kukamatwa na polisi kwa tuhuma ya kushindwa kupanda jukwaani.

Tukio hilo lilivivutia vyombo vya habari si vya hapa nchini pekee, bali duniani kote kutokana na video ya msanii huyo kuwa chini ya polisi kusambaa mitandaoni.

Kosa la kukamatwa kwake ni kushindwa kuburudisha mashabiki waliojitokeza usiku wa Agosti 8 katika ukumbi wa Next Door Arena uliopo Jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Kizz amejitetea kwamba ameshindwa kupanda stejini kutokana na kukosa nguo za kutumbuiza baada ya begi lake la nguo kushushwa kimakosa nchini Kenya badala ya Tanzania.

"Nilipofika Nairobi kutoka Kampala ndege niliyotakiwa kuunganisha nayo ilikua imeshaondoka, nilikaa Nairobi kwa saa nane, nikapata ndege nyingine saa mbili na nusu Usiku, Nilipofika Dar tuligundua kwamba vitu vyangu vimesahaulika, wakasema watanitumia'' amesema Kizz Daniel alipokua akiomba radhi kwa mashabiki zake.

Mratibu wa shoo hiyo ya Summer Amplifed, aliomba radhi kwa umma katika taarifa yake.

Wachambuzi wa mambo ya burudani wamesema, mwanamuziki huyo kutoka Nigeria amekuwa na tatizo la kutopanda majukwaani na kutoa sababu mbalimbali.

Abdul Mfinanga, amesema kitendo cha kukamatwa na polisi na video yake kusambaa duniani kote, imeleta somo kwake kwamba kuna wakati upole unageuka kuwa moto inapobidi.

"Unajua Watanzania wanaonekana kama watu wapole na wasiotaka shida, lakini kwa hili la Kizz Daniel alijitakia mwenyewe kwa sababu hakupaswa kutopanda jukwaani eti hana nguo za kutumbuiza," amesema.

## BASI SAWA

# Desclo awamwagilia moyo mashabiki



MKALI wa Rhumba kutoka nchini Ufaransa, Desclo James, amekata kiu ya mashabiki wa muziki huo baada ya kuachia ngoma yake mpya inayoitwa Juste Une Danse.

Akizungumza na BT mapema wiki hii, Desclo mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), amewashukuru mashabiki wa Rhumba Afrika Mashabiki kwa kuipokea ngoma hiyo inayohamasisha kufanya kazi na kujipongeza.

"Ili tule bata lazima tuwe na pesa kwahiyo tunatakiwa tufanye kazi na kujiburudisha. Wimbo umepokelewa vizuri huko Afrika Mashariki hasa kwenye chaneli yangu ya YouTube," amesema Desclo.

# Hennessyy watakuelewa japokuwa umechelewa

RAPA anayekuja kwa kasi, Hennessyy ameeleza kuna umuhimu kwa wasanii kuisoma na kuielewa mikataba wanayoingia kutokana na mingi kuwa ya kinyonyaji.

Akiongea kupitia East Africa Radio ameeleza kuwa katika label msanii akitaka kuondoka aachwe, bali kwa mtu aliyewekeza ahakikishe anapata faida ya kile alichowekeza.

Msanii huyo ambaye aliwahi kuishi nchini Marekani amewatolea mfano baadhi ya wasanii ambao walikuwa kwenye label tofauti tofauti nchini Marekani kama Nick Minaj na Drake waliokuwa chini ya Lil Wayne na kueleza mikataba mingi huwa miaka miwili mpaka mitatu, inayofika miaka 10 ni kumfunga msanii.





# Kuna funzo kulichowasibu Abdul Kiba, Tunda Man

BAADA ya wanamuziki wa kizazi kipya, Abdul Kiba na Tunda Man, kuomba radhi kutokana na kitendo chao cha kuingia na jeneza katika tamasha la Simba Day, wadau wamejitokeza na kueleza kuna tatizo katika sanaa.

Wakizungumzia suala hilo, baadhi ya watu wamesema wasanii wa muziki ni lazima kutumia akili nyingi katika ubunifu wao na si kutawaliwa na hisia.

"Wengi wa wanamuziki wanatawaliwa na hisia wanadhani kila kitu wanaweza kufanya bila kuangalia athari zitakazotokea, AbdulKiba na Tunda Man wanatakiwa kujifunza kutumia akili," amesema Shukuru Saidi.

# Wakati Ukuta: Jogoo la mjini shamba linachinjwa

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni msemo maarufu sana Tanzania 'Jogoo la Shamba haliwiki mjini.' Waswahili wana maana kuwa mtu yoyote anayetoka kijijini ni lazima atapata changamoto kubwa anapofika mjini kutokana na mazingira anayokutana nayo ambayo ni tofauti na kule alikotoka.

Wa kijijini ni lazima atashangaa vitu vingi ambavyo vitakuwa vipya kwake na vingine hatoweza kuvitumia bila msaada wa mwenyeji.

Lakini kwenye filamu hii ya 'Wakati Ukuta' imekuwa ni tofauti kidogo. Hii sasa ni jogoo wa mjini aliyekwenda kuwika shamba. Akawika hasa, lakini kilichomkuta huko huyo jogoo ni kuchinjwa tu.

Inshu kwenye filamu hii iliyochezwa na kina Luckey Luckano aliyecheza kama Paschal na Stanley Msungu iko hivi. Paschal mtoto wa mjini anayeishi na dada yake, ni kijana mtanashati, lakini hajatulia. Ana tabia ya kutembea na wasichana hovyo, hadi wengine kuwazalisha.

Tabia hiyo inamkera sana dada yake, lakini hana la kufanya na kumfukuza hawezi.

Kuna ndugu yao anafariki huko kijijini. Wote wawili wanakwenda kwenye msiba. Lakini unapomalizika, dada mtu anamwambia Paschal kwanza akae hapo japo kwa mwezi mmoja ili kuzuia uwezekano na baadhi ya ndugu zao kujimilikisha nyumba hiyo pamoja na mashamba ambayo hayawahusu kwenye urithi. Paschal anakubali. Shughuli ndipo inapoanzia.

Utanashati wake unawaduwaza na kuwapumbaza wasichana wengi kijijini na wengine wake wa za watu. Kama kawaida yake, Anaanza kutembea na kila msichana anayejipitisha na kujipendekeza kwake. Lakini mwenyewe rohoni mwake alimpenda msichana mmoja anayeitwa Doroth. Doroth naye akampenda Paschal. Msichana akawa hafanyi kazi kwao. Kutwa kiguu na njia kwa Paschal, kiasi cha mama yake akaanza kuhisi kuna kitu.



Kelele za mama yake Doroth zilimfanya binti amsihi mpenzi wake ajitambulishe kwao, kwani mambo ya kuibana yanasabisha wasilifaidi penzi. Lakini kwa sababu Paschal hakuwa muoaji, aliimdanganya tu ipo siku atajitambulisha tu.

Kila siku kijana huyo alinuka. Tetesi zikawa kubwa kuwa mbali na kuwa anatembea na vibinti vidogo, lakini pia anatembea na wake za watu. Mtego ukawekwa. Siku hiyo Paschal akabambwa anatembea na mke wa Msungu. Kelele kama za mwizi zikapigwa, kila mkazi kijijini hapo akatoka na silaha. Bila kumuangalia mtu usoni, mhalifu akapigwa hadi kufa.

Msiba unafanyika, na baada ya kumalizika tu, Doroth mjamzito. Mama yake kila akimuuliza ni ya nani hajibu. Anaitwa shoga yake Flaviana kuja kumbembeleza, ndipo anapomwambia ni yule kijana aliyeuawa kijijini.





# Joyce kama Rose Mhando mpya

MWIMBAJI chipukizi wa nyimbo za injili Joyce Mabula, amefyatua singo mbili, 'Yesu ni Mzuri' na 'Hatuna Mwingine', ikiwa ni harakati zake za kufikia kilele cha uimbaji.

Joyce ambaye amebainisha kuwa kuingia kwake kwenye Muziki wa Injili kunatokana na kumfutilia sana mama yake ambaye pia ni mwimbaji wa Injili, amesema kuwa kabla ya singo hizo mbili, mwaka 2020 alitoa singo iitwayo 'Mwambie' ambayo ilifanya vema.

"Mama yangu anaitwa Maria Shalom ambaye ana albamu tatu, na baadhi ya nyimbo alimshirikisha Jenifer Mgendi kwenye albamu ya 'Msaada ni Mungu',

# BENDI 5 ZILIZOITIKISA TWANGA PEPETA

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka mwaka 2000 kulitokea mapinduzi makubwa ya muziki wa dansi nchini.

Kuliibuka aina ya muziki ambao uliathiriwa na bendi za Congo DR kama Wenge Musica, Extra Musica na nyingine zinazofanana na hizo.

Aina ya upigaji wao na ziara za bendi hizo hapa nchini ulisababisha kuundwa kwa bendi moja iliyoitwa Diamond Sound wana Kibindankoi ambayo kwa kiasi kikubwa iliiga nyimbo hizo, zingine ikizitoa kwa lugha ya Kikongo na kuziimba kiswahili.

Hili lilipokelewa vema na mashabiki wa muziki wa dansi nchini, kiasi cha kuathiri kidogo bendi zilizokuwa zikipiga rhumba kama Msondo, Sikinde na nyingine.

Miaka michache baadaye ikaundwa bendi inayoitwa African Stars, iliyotumia mtindo wa Twanga Pepeta. Bendi hii ilikuja kutetemesha na kufanya mapinduzi makubwa, kwa kuchukua vionjo vya bendi za Congo DR na kuziimba kiwa kiswahili, wakiongozwa na marehemu Ramdhani Masanja maarufu kama Banza Stone, Ally Choki na wengineo.

Baada ya kulitesa soko la muziki nchini, baadaye ziliundwa bendi zenye mlengo kama huo, ambazo ziliupa ushindani mkubwa Twanga Pepeta na kunyang'anyana mashabiki na kuzua upinzani mkubwa kama wa Simba na Yanga.

**TOT Plus Band**

Ni bendi ya mwanzo kabisa iliyoanza kuitingisha Twanga Pepeta. Kwanza kabisa ilichofanya ni kumchukua kinara aliyekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na kipenzi cha bendi hiyo, Banza Stone.

Kujiunga kwa Banza kwenye bendi ya TOT kulisababisha upinzani mkubwa wa bendi hizi mbili na pia kuipaisha.

Mwanzoni bendi ya TOT ilikuwa ndani ya sanaa za maonyesho na haikuwa inajitegemea yenyewe, lakini kujiunga na Banza kuliifanya bendi hiyo kutoka kwenye kundi hilo la sanaa na kuwa bendi kamili inayojitegemea.

Ikavutia wengi na kuwa mshindani halisi wa Twanga Pepeta.

**Mchinga Sound Band**

Ilianzia mkoani Lindi, lakini ikaja kufanya makazi yake jijini Dar es Salaaam. Ni bendi ambayo nayo ilikuja kuisumbua mno Twanga Pepeta, kwa sababu iliwachukua baadhi ya wanamuziki wake kama Adolf Mbinga, Joseph Watugulu, Rogat Hega 'Katapila' na wengineo.

Hali hii ilisababisha mashabiki wa Twanga Pepeta kuiona si bendi rafiki kwao na kukawa na upinzani mkali si kati ya bendi hizo mbili tu, bali hata uongozi wa bendi hizo mbili nao mara kwa mara ulikuwa ukiingia kwenye mzozo wa kila moja kudai kuifanyia njama ya kuidhohofisha bendi nyingine.

**Chuchu Sound Band**

Kama kuna bendi ambayo ilikuja kwa kasi na kuondoka kwa kasi vile vile ni hii. Chuchu Sound ni bendi ndogo tu ambayo iliundwa na baadhi ya wanamuziki wa Kikongo na Kitanzania, lakini ilitesa na kuzoa mashabiki wengi kwa muda mfupi na kuziacha bendi nyingine, ikiwemo Twanga Pepeta zikiulizana.

Sababu ni staili yao. Ilikuja na aina mpya ya muziki ambao ulikuwa ni wa kimwambao maarufu kama 'mduara' uliokuwa ukihanikizwa na vionjo kutoka kwa wanamuziki kama Omari Mkali, Chuchu Yusuph mwenyewe, Mao Santiago, Jenico Flower na wengineo.

Ilipiga muziki wa aina zote, kama wa bendi za Twanga Pepeta, lakini mduara ndiyo ulioibeba zaidi.

**FM Academia**

Baada ya kuipa changamoto Diamond Sound Band, wakati huo ikiitwa FM Musica, ilibadisha jina na kujiita FM Academia. Sasa ikahamia kuipa wakati mgumu Twanga Pepeta, ikiwa na kina Nyosi El Sadaat. Ni bendi ambayo kwa kipindi kirefu imetoa ushindani mkubwa kwenye muziki wa dansi nchini hasa wa kizazi hicho kuanzia mwishoni mwa miaka ya '90 hadi leo.



# Ada Ameh kuzikwa nyumbani kwao

MWILI wa mwigizaji mkongwe wa Nollywood, Ada Ameh, utazikwa katika eneo alilozaliwa la Benue nchini Nigeria.

Kulingana na mipango ya mazishi iliyotangazwa na familia yake, katika mazishi hayo itatanguliwa na ibada ya kuwasha mishumaa, na itafanyika kwa heshima yake.

Ameh alifariki Jumapili, akiwa na umri wa miaka 48 baada ya kuanguka ghafla nyumbani kwake.



## Charly Boy utabiri gani huo?

MWANAMUZIKI wa siku nyingi kutoka Nigeria, Charles Oputa, maarufu kama Charly Boy, ametabiri kutokea kwa majanga endapo viongozi aliowaita wahuni watatawala nchi hiyo.

Mkongwe huyo wa muziki kupitia ukurasa wake wa Twitter, amesema nchi hiyo itakuwa kama Afghanistan, Venezuela na Somalia kama aina hiyo ya viongozi watapewa madaraka.

“Ikiwa Wahuni walio madarakani watabaki na kutojali au kushindwa kurekebisha hali hiyo hakika Nigeria itakuwa mchanganyiko wa Afghanistan Venezuela, Somalia na Lebanon, “ alitweet.

## Lavato weka wazi wamjue

MKALI wa muziki wa Marekani Demi Lovato, anaripotiwa kuwa katika uhusiano mpya wa kimapenzi.

Kulingana na PageSix, mwimbaji huyo anachumbiana na mwanamuziki ambaye bado hajajulikana.

“Ni uhusiano wenye furaha na afya, yeye ni mtu mzuri,” mtu wa karibu wa mwimbaji huyo aliuambia mtandao huo.





## Kim si kwa mahasira hayo!

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha maisha halisi katika televesheni nchini Marekani, Kim Kardashian anasemekana kukasirishwa na aliyekuwa mume wake, Kanye West, baada ya kutoa maoni kuhusu yeye kutengana na mpenzi wake Pete Davidson.

Kulingana na PageSix, mama huyo wa watoto wanne hajafurahishwa na majibu ya Kanye ambaye alizungumzia kutengana kwao.

“Kim amekasirika sana. Kanye amerudi kwenye njia zake za zamani na Kim hatavumilia tabia yake ya uonevu kwa watu anaowapenda na kuwajali,” chanzo kilieleza.

Haya yanajiri saa chache baada ya Kanye kupost kwenye ukurasa wake wa Instagram, akimkejeli Davidson.

## Okeke kutoa talaka si suluhu

MWIGIZAJI wa Nollywood, Gideon Okeke, na mkewe Chidera imeelezwa wako hatua ya mwisho kupeana talaka.

Kwa mujibu wa chanzo kilicho karibu na wanandoa hao, wanakaribia kukatisha ndoa yao ya miaka minne kutokana na tofauti zisizoweza kusuluhishwa.

Familia ya Okeke itakwenda kijiji cha Chidera kuchukua mahari aliyolipwa wiki iliyopita, chanzo kilifichua.



# Hali ngumu ya maisha yatajwa maficho WAVIU kukatiza ARV

## ■Kampeni yawarudisha kwenye mstari

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya kuongezeka kwa kiwango cha kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa wanaoishi na virusi hivyo (WAVIU) wanaotumia dawa kutoka asilimia 87 mwaka 2016 hadi asilimia 92 mwaka 2019, hali duni ya maisha imetajwa kuwa moja ya vikwazo vinavyochangia WAVIU kukatiza matumizi ya dawa hizo.

Hayo yanajiri wakati Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) ikibainisha vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua kutoka 64,000 mwaka 2010 hadi vifo 32,000 mwaka 2020 wakati maambukizo mapya ya VVU yameshuka kutoka watu 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020.

Vilevile, tangu kuibuka kwa janga jipya la maambukizo ya virusi vya corona mwaka 2019, imeelezwa kuwa uchumi katika kaya mbalimbali umeyumba na kusababisha baadhi ya WAVIU kukosa ari au hamasa ya kutumia ARVs na kuwekeza nguvu kubwa katika kujitafutia kipato.

Katika kukabiliana na shida hiyo, Kampeni ya GGM Kili Challenge iliyoasisiwa mwaka 2002, imeelekeza nguvu katika kuwasaidia WAVIU kupitia asasi za kiraia ambazo zinajishughulisha na udhibiti wa maambukizo ya VVU na Ukimwi kwa namna mbalimbali.

Asasi hizo zimekuwa zikiyafikia moja kwa moja makundi hayo ya WAVIU ambao wengi wao ni kinamama, vijana na watoto na kuwawezesha kupitia vikundi mbalimbali walivyoviunda.

Kampeni hiyo ambayo iliasisiwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na TACAIDS, imeendelea kuwa msaada mkubwa kwa asasi hizo, hasa ikizingatiwa kuwa tangu kuasisiwa kwake, fedha nyingi zimekusanywa na kuelekezwa kwenye Mfuko wa Kudhibiti Ukimwi pamoja na asasi hizo kwa ujumla.

Kampeni hiyo inalenga kukusanya fedha kila mwaka ili kuchangia juhudi za serikali kufikia malengo ya sifuri tatu kwa maana ya kufikia asilimia sifuri katika maambukizo mapya, sifuri ya unyanyapaa na sifuri katika vifo vitokanavyo na UKIMWI. Mwaka 2020 pekee, kampeni hii ilikusanya na kugawanya jumla ya Sh. milioni 800 kwa asasi mbalimbali nchini.

### AGAPE - NJOMBE

Moja ya asasi zinazofaidika na kampeni hiyo ni Kituo cha AGAPE - Njombe ambacho msimu uliopita kilipata ruzuku ya Sh. milioni 29.9 kutokana na andiko walilowasilisha kwenye timu ya wataalamu wa GGM Kili Challenge.

Mratibu wa Kituo hicho, Enara Nyagawa, anasema fedha hizo zimewasaidia kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa watoto na familia zinazoishi na VVU.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai (wa pili kulia) na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule (katikati), wakipokea bendera kutoka kwa mmoja wa washiriki wa Kampeni ya GGM Kili Challenge waliopanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kuchangia fedha za kuendeleza mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Wanufaika hao ni kutoka maeneo mbalimbali ya Njombe, Kibena na Iyombo, ambao wameanzisha miradi mbalimbali ya ujasiriamali kutokana na ruzuku wanazopatiwa.

Anabainisha kuwa WAVIU 128 wamefikiwa katika mradi huo huku wahitaji wengi wakibaki bila kupata kitu, jambo ambalo anashauri nguvu kubwa ielekezwe katika kutunisha mfuko huo ili kuinua maisha ya watu hao.

### KONGA - TEMEKE

Asasi nyingine ambayo imefaidika na fedha za mfuko huo wa GGM Kili Challenge ni pamoja na Taasisi ya Konga - Temeke ambayo mradi wake umeelekezwa katika Manispaa ya Temeke iliyoko mkoani Dar es Salaam.

Katibu wa Mradi wa taasisi hiyo, Japhes Mulokozi, anasema mradi wao ambao ulipata Sh. milioni 28.9, ulilenga kuwajengea uwezo WAVIU kwa njia mbalimbali ili kujipatia kipato na kuzihudumia familia zao.

Anasema zimetumika kukopesha vikundi zaidi ya 15 ambapo kila kikundi kimepata Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha shughuli za ujasiriamali.

Anasema mbali na mikopo hiyo, pia wametoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa wanakikundi hao, hasa ikizingatiwa kuwa wanawake, hususan vijana wa kike ndiyo waathiriwa wakubwa wa VVU kwa kuwa baadhi yao hujiingiza kwenye biashara haramu ya ngono pindi wanapokosa fedha za kujikimu.

Anasema vikundi hivyo vinatakiwa kurejesha mikopo hiyo ndani ya miezi mitatu kisha kuwapatia wanakikundi wengine ambao nao wanahitaji fedha hizo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

"Tatizo kubwa hapa tunaona fedha ni kidogo na kwamba hazitoshi kwa sababu waliojitokeza kujisajili kwenye mradi ni zaidi ya 50 lakini tumeweza kufikia vikundi 20 pekee hadi sasa," anasema.

### MTWARA

Asasi nyingine iliyofanikiwa kupata fedha zilizotokana na kampeni hiyo ya GGM Kili Challenge ni Volunteer for Youth in Health and Development ya mkoani Mtwara ambayo ilipata Sh. milioni 30.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Deogratius Makoti, mradi waliopatiwa fedha umewasaidia kuinua kiwango cha matumizi ya ARV kwa waathirika wa VVU hususani katika eneo la Nanyamba mkoani huko.

Anasema wakati mradi huo unaanza mwaka mmoja uliopita, jumla ya WAVIU 47 waliripotiwa kuwa wameacha dawa za ARV lakini baada ya mradi huo kuanza, wote wameendelea na dawa.

Pia anasema wakati mradi unaanza jumla ya WAVIU 50 walikuwa na ufuasi mdogo wa ARV, akiwa na ufafanuzi kwamba walikuwa wanatumia leo baada ya siku kadhaa wanaacha na baadaye wanarejea tena kutumia, lakini wote hao walirejeshwa na kuanza kutumia tena dawa kwa usahihi.

"Mafanikio yote hayo yametokana na mikopo ambayo tulitoa kwa vikundi ambapo sasa hata wale sugu kwa matumizi ya dawa wakawa wanakutana na wazoefu wa kutumia dawa kwenye vikundi vyao kisha kupata elimu ambayo iliwahamasisha kuhakikisha wanakuwa na ufuasi wa dawa mzuri.

"Hivi sasa ukikagua zile CTC kadi, WAVIU wengi wamepewa dozi za miezi mitatu kwa maana kuwa mtiririko wake wa kutumia dawa umeimarika. Mgonjwa akipewa dawa za mwezi mmoja ina maana kuwa ufuasi wake wa kutumia dawa ni wa kusuasua.

"Ndiyo maana tunaweza kusema mradi huu tumeutumia kuwaokoa kutoka kwenye ufuasi mbovu wa matumizi ya ARV na sasa tumewafikia WAVIU 388 kupitia kwenye vikundi vyao na kuwatambua wenye shida," anasema.

Anabainisha kuwa vikundi vingi vinakumbwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo mahitaji ya fedha kuwa mengi.

"Lakini pia kuna tatizo la menejimenti ya kusimamia vikundi, ndiyo maana baadhi yao vinasambaratika kwa sababu tu mtu mmoja au wawili wanaona kama wamewekwa pembeni au gawio ni dogo.

"Lakini sasa tumewapa mafunzo ya usimamizi wa fedha kwenye ujasiriamali, tukawafundisha namna ya kutengeneza vitu ambavyo wanauza wenyewe, mfano vikapu, bidhaa zenye soko vijijini, siagi, divai za mabibo na mananasi pamoja na utengenezaji wa batiki, crisp za ndizi na viazi," anasema.

Alisema tatizo kubwa linalowakabili mbali na uhaba wa fedha zinazotakiwa kuwafikia WAVIU wengi zaidi, ni baadhi ya idara za serikali kutotoa ushirikiano wa kutosha katika kuwajali WAVIU pindi wanapohitaji kushiriki katika maonyesho mbalimbali.

### REKODI YA GGM

Kupitia kampeni hiyo mwaka huu, GGML imeendelea kuweka rekodi ya kipekee katika mchango wake kwenye utoaji wa huduma za kijamii baada ya kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.1 kupitia kampeni ya GGM Kili Challenge 2022.

Kampeni ya mwaka huu ilikuwa na washiriki 52 ambao kati yao, 28 walipanda Mlima Kilimanjaro kwa kutembea kwa miguu na 24 kwa kuuzunguka kwa kutumia baiskeli kupitia lango la Machame na kushukia lango la Mweka.

Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, anasema kampeni ya mwaka huu imekuwa na mafanikio ya kipekee.

Anasema kampeni hiyo ambayo ilizinduliwa rasmi Juni 29 jijini Dodoma na kufuatiwa na harambee ya uchangiaji wa fedha iliyofanyika Julai 14 kisha Julai 15 washiriki wakaagwa kwa ajili ya kupanda mlima, pia ilihusisha utoaji wa huduma za upimaji, uchangiaji wa damu na utoaji wa chanjo bure dhidi ya UVIKO-19 kwa wakazi wa Mji wa Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

"Kampeni ya mwaka huu imehusisha pia shughuli za utoaji wa huduma mbalimbali kuanzia lango hili la Machame, Kialia, Soko la Kalali na Nshara na sasa hapa Mweka. Mojawapo ya huduma hizo ni utoaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19, uchangiaji wa damu, upimaji wa VVU kwa hiari na utoaji wa huduma mbalimbali za masuala ya afya ya uzazi.

"Nina furaha kubwa kuwaeleza kuwa katika huduma hizo zilizoanza kutolewa kuanzia tarehe 15 hadi 18 Julai mwaka huu, jumla ya watu 463 wamepimwa VVU ambapo majibu yameonyesha kuwa wote hawana maambukizo ya virusi hivyo. Vivyo hivyo watu 411 wamejipima wenyewe kwa hiari. Hii ni hatua kubwa sana katika mwitikio wa Watanzania kutaka kujua hali ya afya zao," anasema.

Pia anasema katika utoaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19, wataalamu wamefanikiwa kutoa chanjo kwa watu 822 ambao kati yao, wanaume ni 365 na wanawake ni 427 wakati katika uchangiaji wa damu zimekusanywa chupa 27 za damu na katika ugawaji wa kondomu, jumla ya mipira ya kiume 9,335 na ya kike 200 imegawiwa kwenye maeneo hayo.

"Pia, ili kutoa elimu ya kutosha kwa umma kuhusu masuala ya VVU/Ukimwi, katika msimu huu wa Kampeni ya GGML Kili Challenge, tembe za PrEP ambazo ni mahsusi kwa matumizi ya kupunguza makali ya VVU na kwa watu wasio na VVU ili kuzuia upatikanaji wa maambukizo ya VVU ziligawiwa na vipeperushi 204 vya masuala ya afya ya uzazi viligawiwa pia," anasema.

Akizungumza katika mapokezi ya wapanda mlima mwaka huu yaliyofanyika Julai 15, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro wakati huo, Stephen Kagaigai, aliwapongeza washiriki hao 52 waliopanda Mlima Kilimanjaro, akiwaita mashujaa.

Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko,

anatoa wito kwa wadau wengine kukaa mezani na taasisi hiyo ili kupeana mbinu za kuchangisha fedha zaidi kutunisha Mfuko wa Kudhibiti Ukimwi nchini.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...



Na Adam Fungamwango

# Unakumbuka kindumbwendumbwe chalia?

## ■Ngoma ya watoto vikojozi, ikawa maarufu dansini
## ■Msemo ukachukuliwa na wanamichezo



KUKIWA na mechi kubwa kama ya Simba na Yanga hivi leo, watangazaji, wachambuzi na hata mashabiki wa mtaani utasikia wakisema "leo kuna kindumbwendumbwe."

Hata hivyo si wengi hasa vijana wa kizazi cha sana wanaojua maana ya msemo huo. Wao wanajua neno lenyewe lilivyo, lakini sidhani kama wanajua limetokea wapi na kwa nini.

'Kindumbwendubwe' ni ngoma ya watoto zamani ambayo walikuwa wakiipiga kwa ajili ya kumuadhibu mtoto mwenzao ambaye ana tabia ya kukojoa kitandani usiku.

Adhabu hiyo haikuwa inatolewa na watoto, bali wazazi wenyewe. Niliwahi kusema huko nyuma kuwa wazazi wa zamani walikuwa na tabia zinazofanana. Anavyolelewa huku, ndivyo hivyo hivyo atalelewa na nyumba zinazofuata zote na hata mtaa mzima.

Mzazi mwenye mtoto kikojozi siku hiyo, atawaita watoto wenzake mtaani hapo. Nao kwa kujua kuwa wanakwenda kumfanyia kitu mwenzao kikojozi, hakuna urafiki siku hiyo. Watakuja na ngoma na mabati. Wataanza kupiga na kuimba wimbo maarufu sana wakati huo.

"Kindumbwendumbwe chalia, kindubwendumbwe chalia, kikojozi na nguo kaitia moto eee..." Wimbo huo utarudia hivyo hivyo hadi zoezi likamilike. Kwenye kumpigia ngoma kikojozi hakuna ngoma nyingi kama kwenye harusi, disco au kwenye shughuli zingine za kijamii. Ni kama kinamama kisasa wa uswazi anavyokwenda kumsuta mwenzao. Huwa hakuna nyimbo nyingi. Utofauti uliopo ni kwamba wanaokwenda kumsuta mwenzao wanamfuata nyumbani kwake na kumpigia hapo hapo hadi wanaondoka. Lakini kindumbwendubwe, mtoto kikojozi atalazimishwa na wazazi au mzazi mmoja kukusanya mkeka wake, au godoro na shuka, wakimlazimisha kubeba na kutembea na mzigo huo mtaa mzima, huku kundi la watoto kikiwa nyuma yake, wakiwepo wapigaji na waimbaji.

Wakati mwingine anavishwa makopo na matambara mabovu.

Kwenye miji mikubwa na ambako hakuna mto, mtoto huzungushwa mitaa kadhaa kabla ya kurudishwa nyumbani, akiwa hoi bin taaban.

Kwenye miji, vijiji au sehemu zenye mito, au mabwawa, mtoto atapelekwa hadi huko, ataogeshwa kwa nguvu na kulazimishwa kufua shuka zake, na kusafisha mkeka wenye mikojo na baada ya hapo kurudishwa nyumbani na ngoma hadi anafika, akiwa amechoka sana.

Miaka ya 1990 kurudi nyuma, ilikuwa haipiti siku mbili bila kusikia vigoma vya kindumbwendubwe ambavyo mara nyingi vilikuwa vikisikika kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi. Ikifika saa tano huwezi tena kusikia. Huwezi kusikia chochote kuanzia mida hiyo, basi ujue siku hiyo hakuna mtoto aliyekojoa kitandani hapo jirani.

Uchunguzi wangu mdogo uligundua kuwa watoto wengi waliokuwa wanapigishwa kwata hiyo ya kindumbwembwe ni kuanzia miaka saba hadi 10 kwa sababu walikuwa tayari wana uwezo wa kujua kuamka wenyewe usiku na kukojoa, lakini pia uwezo wa kuamka usiku kabla hawajajikojolea.

Hali hii ilikuwa ikizunguka kama pesa za upatu, leo utasikia kindumbwendumbwe huku, kesho kwa mtoto mwingine ambaye jana alimpigia mwenzake ngoma.

Kingine ni kwamba sikuwahi kusikia mzazi hata mmoja wakati huo akikataza kitendo hicho. Wao waliamini ndiyo ilikuwa njia pekee ya kuwafanya watoto wao waache kukojoa kitandani.

Kilichokuwa kinafanyika hapo ni kumfanya mtoto aone aibu mbele ya watoto wenzake na rafiki pia ili kesho yake asirudie tena.

Tukio lile hadi mwisho lilikuwa ni sawa na kwata kabisa, kwani hata kama anagoma alilazimishwa kutembea hadi anafika mtoni au kuzungushwa kote na kurudishwa. Ila cha ajabu ni kwamba hawakuwa wanapigwa. Na wazazi walisisitiza kuwa wanaofanya kazi ile wasimpige mwenzao, kwa hiyo ikawa kama kanuni hivi.

Na sijawahi kusikia mtoto kagoma kuzungushwa mtaani, au kupelekwa mtoni, au kufika njiani katoroka na kuwakimbia wenzake. Inaonekana watoto wa zamani walikuwa watiifu sana, ingekuwa sasa huko njiani akibaki na watoto wenzake, pangechimbika.

Kwa kiasi kikubwa ilisaidia baadhi ya watoto kuacha, hasa wale wazembe, au wanaofanya makusudi, lakini wachache kati yao ilikuwa kazi bure.

Nadhani wazazi wa wakati huo hawakuwa na uelewa mpana sana kuwa baadhi ya watoto walikuwa na ugonjwa. Yaani pamoja na kwamba walikuwa sahihi kwa wakati huo, lakini kuna wengine walikuwa wagonjwa. Na ndiyo hao hata uwafanye vipi kesho wanakojoa tena.

Haijulikani mpaka sasa ni nani hasa mtunzi wa wimbo ule wa kindumbwendubwe, ni watoto wenyewe au mtu mzima, lakini ulikuwa maarufu mno.

Jina la wimbo huo lilichukuliwa na bendi ya muziki wa dansi iliyovuma mwanzoni mwa miaka ya 1990, Bicco Stars chini ya uongozi wa Ramadhani Kinguti 'System', ikiwa na wanamuziki kama Fresh Jumbe, Asia Daruwesh, Andey Swebe na wengine. Ikaanza kutumia mtindo wa 'Kindumbwendubwe Chalia.' Ukawapatia umaarufu mkubwa.

Hata watangazaji na wachambuzi wanapotaka kuonyesha kuwa kuna pambano kali na la kukata na shoka, basi watasema kuna kindumbwendubwe. Au timu ambayo imefungwa mabao mengi, watasema imechezeshwa kindumbwendumbwe, wakinasibisha na msukosuko waliokuwa wakipata watoto wa zamani waliokuwa vikojozi ya kutembezwa mitaani, na kupelekwa hadi mtoni asubuhi na mapema.

Wakati naandaa makala hii na kuiweka kwenye mtandao, wapo wadau walioona, au kukumbana na madhila haya wakachangia.

"Umenikumbusha mbali 'kindumbwendumbwe chalia', yaani mtoto anavishwa matambara na kufungwa makopo, anazungushwa mitaani huku watoto wenzie wakimzomea ili asikojoe kitandani tena. Ina maana wazee wetu walikua hawajui kuwa huu ni ugonjwa?" Akakumbuka na kuhoji mchangiaji mmoja.

Mama mmoja yeye akaandika kwa hisia kali.

"Kukojoa kitandani,hili sitasahau. Unakojoa halafu asubuhi unapigiwa kindumbwendumbwe na makopo unapitishwa mitaa yote, ilikuwa balaa ya ajabu. Siku hizi jamani tumestaarabika hata kama mwanao anakojoa unampa ushauri na kumsaidi kumuamsha akakojoe nje, lakini zamani, looo... ilikuwa balaa jamani acha tu."

Mmoja akataka eti watoto wa sasa nao wafanyiwe hivyo.

"Lengo langu ni kuwa hata sasa watoto wengi wanakojoa kitandani wafanyiwe hivyo."

Mchangiaji mwingine akamjibu.

"Jaribu leo hii kumfanyia mtoto wako hiyo, dunia hii ya leo hii yenye Haki za Mtoto na Binadamu, utaishia pabaya. Pia wazazi wa sasa wanawadekeza sana watoto huwezi kukuta hili, yameisha na zama zimepita, kila kitabu na zama zake."

Yupo mmoja akajitambulisha kuwa yeye alikuwa kikojozi wakati akiwa mdogo.

"Nakumbuka nilipokuwa mtoto nilikuwa nakojoa kitandani, baba akanipiga mkwala kuwa atanifanyia kindumbwendumbwe, mbona niliacha kukojoa. Sidhani kama siku hizi inawezekana tena, wabongo wako bize na mambo yao tu, maisha yamekuwa magumu ya kutafuta sana, hata watoto wanajua hilo ndiyo maana hawawezi kufanya hivyo tena kuzungushana mitaani wakati hawajanywa hata chai..." Akamalizia mchangiaji huyo.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Waliofutwa ubunge washinda kesi kortini

**Na Waandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imewapa ushindi wabunge wanane na madiwani wawili wa Viti Maalum CUF waliovuliwa uanachama na kupoteza nafasi zao kwa sababu chama hicho kilivunja Katiba yake na hakikuwapa nafasi ya kuwasikiliza.

Hao ni Miza Bakari Haji na wenza saba na Diwani Elizabeth Magwaja na mwenzake, ambao hukumu ya kesi yao ilitolewa jana na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam mbele ya Jaji, Dk. Juliana Masabo baada ya kupitia hoja zilizowasilishwa na pande zote mbili zinazopingana.

Jaji Masabo alisoma hukumu ya kesi namba 143 ya mwaka 2017 iliyofunguliwa na Miza Bakari Haji na wenzake tisa dhidi ya CUF, Spika wa Bunge, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Manispaa za Ubungo na Temeke, wakipinga kufukuzwa uanachama na hatimaye ubunge na udiwani wa viti maalum kupitia CUF.

Pamoja na kuwashitaki hao, wabunge hao pia waliwashitaki waliochukua nafasi zao za ubunge baaada ya kuvuliwa ambao ni Rukia Kassim, Shamsia Mtamba, Kiza Mayeye, Zainabu Mndolwa, Hindu Mwenda, Sonia Magogo, Afredina Kahigi na Nuru Bafadhili.

Waliokuwa wabunge ni Miza Haji, Savelina Mwaijage, Salma Mwassa, Raisa Mussa, Riziki Shabani Ngwari, Hadija Salum Ally Al-Qassmy, Halima Mohammed, Saumu Sakala na madiwani ni Elizabeth Magwaja na Layla Madibi. Akisoma hukumu hiyo, Jaji Masabo alisema baada ya kupitia mawasilisho, mahakama inatamka kwamba CUF ilivunja Katiba yake na ilivunja haki za wadai kwa kuwafukuza uanachama bila kuwapa nafasi ya kusikilizwa.

Mahakama hiyo pia ilisema CUF iliwavua uanachama wadai kabla mchakato wa rufani zao walizokata kupinga kufukuzwa uanachama kuwa zimesikilizwa ndani ya chama.

"Mahakama imezingatia ushahidi kadhaa, ikiwamo kukiri kwa CUF yenyewe katika utetezi wake kuhusu mambo kadhaa, ikiwamo haki ya kikatiba ya kukata rufani.

"Mahakama Kuu inatamka kwamba Spika na Tume ya Uchaguzi hawana hatia kwani wao walipokea tu taarifa kutoka CUF kuhusiana na wadai ya kufukuzwa uanachama wao," alisema Jaji Masabo.

Hata hivyo, mahakama iliamuru kila upande utabeba gharama zake za kuendesha shauri husika. Wabunge hao walikuwa wakiwakilishwa mahakamani na Wakili Peter Kibatala.




Basi la wafanyakazi la kampuni ya Jambo Food Product, lenye namba za usajili T 841 DHY, likiwa limeteketea kwa moto, eneo la Bugweto, Manispaa ya Shinyanga jana, baada ya kutoka kusafirisha wafanyakazi waliokesha kazini. Dereva wa gari hilo, Silvester Derefa, alinusurika katika ajali hiyo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Zimamoto watangaza mabadiliko tozo ukaguzi

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limetangaza mabadiliko ya tozo za ukaguzi wa usalama dhidi ya majanga ya moto katika majengo na maeneo mbalimbali.

Vilevile, limetangaza maingizo mapya ya tozo sehemu za karakana, vituo vya usafirishaji na wafua nguo (dry cleaner).

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Puyo Nzalayaimisi, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi, alisema tozo hizo zinakusanywa kwa mujibu wa sheria namba 14 ya mwaka 2007.

Alisema kuwa awali Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilikuwa na jukumu la kumfuata mteja na kuomba kufanya ukaguzi katika jengo, eneo au chombo cha usafiri.

Alisema utaratibu huo kwa sasa umeboreshwa ili kuleta tija na kuliwezesha jeshi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

"Kwa mujibu wa kanuni ya ukaguzi na vyeti ni wajibu wa mteja kufika kwenye vituo na ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mikoa yao ili kuweka mpango kazi wa kukaguliwa. Wakati huo bado tunaendelea kuboresha mifumo yetu ili wateja wetu wapate nafasi ya kuomba kupitia mtandao," alisema.

Nzalayaimisi alisema mabadiliko ya gharama za tozo katika maeneo kama maduka, viwanda, makazi, ofisi, shule, nyumba za kuishi yanaambatana na usomaji wa ramani, gharama za usajili wa kampuni zinazojishughulisha na utoaji wa kuuza vifaa, uwekaji wa vifaa vya kuzima moto pamoja na mifumo ya uzimaji moto.

Hata hivyo, alisema kushuka kwa gharama hizo kuna maingizo mapya ya tozo ikiwa ni pamoja na sehemu za karakana, vituo vya usafirishaji na wafanyabiashara ya kufua nguo.

Alizitaja tozo zilizofutwa kuwa ni pamoja na tozo za transforma, mashamba ya kahawa, mkonge na chai.

Kamishina huyo aliwataka wamiliki wa majengo, maeneo pamoa na vyombo vya usafiri kufuatilia taarifa ili kupata elimu, sheria na nyaraka nyingine kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii.

Alisema tozo kwenye maduka ambapo awali walikuwa wanalipa Sh. 40,000, kwa sasa yamegawanywa katika makundi mawili, rejareja ambao wanalipa Sh. 20,000 na jumla ambao wanalipa Sh. 30,000.

Alibainisha kuwa kwa wakulima zimeondolewa kabisa, ambapo awali walikuwa wakilipa kuanzia Sh. 500,000 kulingana na ukubwa wa shamba.

Kwa upande wa wachimbaji wadogo ambao awali walikuwa wakilipa Sh. milioni sita , tozo hiyo imeshushwa kulingana na mita za mraba ambapo kuanzia sifuri hadi 200 wanalipa Sh. 100,000 na mita za mraba 2,001 hadi 4,000 wanalipa Sh. 400,000.

■**Imeandaliwa na Magdalena Jackson na Peter Mkwavila**

# Posta kutumika kutoa mikopo elimu ya juu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC) limeingia mkataba na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ili kuwarahisishia wanaoomba mikopo, wapate kwa urahisi bila usumbufu baada ya kujaza nyaraka zote muhimu zinazotakiwa.

Posta pia, imeanza kutoa huduma kwa wananchi wanaohitaji vyeti vya kuzaliwa ambapo kazi ya kujaza fomu na nyaraka zote inafanyika posta na mwananchi akikamilisha taratibu zote, anakwenda kwa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kuchukua cheti tu.

Meneja wa TPC Mkoa wa Singida, Michael Mwanachuo, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema shirika hilo limeanza kutoa huduma hizo ili kurahisisha na kupunguza usumbufu kwa wananchi.

Alisema Posta inawasaidia wanafunzi kufanya maombi kwa mtandao na baada ya kukamilisha kujaza fomu zao wanatakiwa waende katika ofisi za Posta ili kuzituma kwenda HESLB.

"Hivi sasa tatizo la wanafunzi kukosa mikopo kwa sababu ya kukoseakosea halitakuwepo, mhusika atakuja Posta atasaidiwa namna ya kujaza fomu zake kwa usahihi kabisa," alisema.

Kuhusu vyeti vya kuzaliwa, Mwanachuo alisema shirika limeanza kusaidia kutoa huduma hiyo ambapo waombaji wanajaza fomu kwa njia ya mtandao ambapo Posta inawasaidi na taratibu zote zikikamilika wanakwenda RITA kuchukua vyeti vyao.

Meneja huyo aliwaalika wananchi na wanafunzi kufika Posta kupata huduma hizo ambazo zinatolewa kwa haraka na kwa ufanisi zaidi ili kuliunga mkono shirika hilo.

Hivi karibuni serikali kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ilisema taasisi zote za kiserikali zitaanza kutoa huduma zote ndani ya ofisi moja.

Mpango huo ni mkakati wa muda mrefu wa serikali katika kuziunganisha taasisi za kiserikali kufanya kazi kwenye ofisi moja.

Wizara ya, Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeweka mikakati katika kusimamia mifumo ya kidigitali ili kupunguza usumbufu kwa wananchi pindi wanapotaka huduma kwa uharaka zaidi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA BUKOBA**
**MAOMBI NA 12/2022**
**YANAYOTOKANA NA KESI YA KUHUJUMU UCHUMI Na 14/2011**
**Ya**
**Resident magistrate Court Bukoba)**
**DIRECTOR OF PUBLIC ROSECUTION ............MUOMBAJI**
**DHIDI**
**YASIR AZMI**
**RESPICIUS ABEL RUCHANGULA}**
**WAJIBU MAOMBI AFIDHU ABDUL KALUGIRA}**

**WITO/KUITWA SHAURINI.**

**Kwa' YASIR AZMI**
**Popote ulipo**
Hii nikukutaarifu kwamba shauri la Mambi ya rufaa tajwa juu imepangwa Kusikilizwa tarehe 18 mwezi Agosti mwaka 2022 saa 3.00 asubuhi, mbele ya MH.Jaji KILEKAMAJENGA wa Mahakama Kuu, Kanda ya Bukoba.

Kwa hiyo, unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria.

Endapo hutohudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi Wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.
**Imetolewa kwa mkoni wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 9 mwezi Agosti mwaka 2022.**

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**BUKOBA.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**WILFRED NDESAMBURO SWAI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 841 ABA.** Chasses Namba **RN 40-105128,** Engine Namba **12R 2526311** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . **Polisi Taafifa : KIL/MOS/RB/311870/2022**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya BUKOBA**
**BUKOKA MJINI**
**Kituo cha BUKOBA MJINI**
**Shauri la Miradhi NA.44/2017**
**Jina la msimamizi JOHN GONZA NDIBALEMA**
**Jina la marehemu: NATHANAEL NDIBALEMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuniya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)

Kwa **JOHN GONZA NDIBALEMA** Kwa kuwa mdai/wadai wa meleta/wameleta madai yake.Kwa kuwa **BI IENA NCHOCHENA** ameomba **JOHN GONZA NDIBALEMA** atenguliwe usimamizi wamirathi ya marehemu **NATHANAELI NDIBALEMA** kwa hiyo unatakiwa
Kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 22 mwezi 8 mwaka 2022 saa 2 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo.na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shaur ihili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakam a inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo .
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo terehe 27 mwezi 7 mwaka 2022.

............................
**HAKIMU**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MPANDA**

**Kituo cha MPANDA Mkoa wa KATAVI**

**Shauri la Madai Na, 101 /2022**

**Jina la Mdai RAMADHANI KASONSO**

**Jina la Mdaiwa (1) VITALISI KASONI (2) RAFAEL NYAMBO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za Utaratibuwa Madai katika Mahakama za Mwanzo )**

**Kwa RAFAEL NYAMBO WA MAKANYAGIO**

**Kwa kuwa Mdai/ Wadai ameleta madai /yao kwamba ( Eleza habari za Madai)**

**MADAI YA FEDHA TSHS 4,200,000/=** kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 Mwezi 08 Mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi /Mchana kwa mujibu wa madai hayo kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea .
**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo .

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi wa 08 Mwaka 2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**CATHERINE LEONARD AKWILAPO** anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJ** yenye jina City Boys Electronics Company Ltd aina ya TVS yenye namba za usajili **MC 952 CBL.** Chassis no. **MD6M14PA5J4K63141,** Engine no. **AK4K14274724.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/311693/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **MICHALE JOSEPH GWACHO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Grader lenye namba za usajili **T289 BFM,** injini namba **6D10521** na Chassis namba **GD405A21382.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/319764/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0711265777.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ROGATHE ELIA MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SCANIA TIPPER TRUCK** yenye namba za usajili **T839 AFV** chasis namba **1138673,**engine namba **5083060,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochotye cha polisi Polisi taarifa **DAR/OST/RB/319801/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MAHESH KUMAR LEKHRAM** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Toyota NOAH yenye namba za usajili **T329DEL,CHASSIS NO AZR603003287,ENGINE NO 1AZ5339296** Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi cha karibu. **Taarifa polisi:- ARU/ARU/RB/320542/2022.**

**WILAYA YA KILINDI**
**MAOMBI MADOGO NA.46 YA MWAKA 2021**
**JUMA WAZIRI ................................MSHINDA TUZO**
**DHIDI YA**
**MNYAMISI KIONDO..........................MSHINDWA TUZO**

**KWA MSHINDWA TUZO,**
**MNYAMISI KIONDO POPOTE PALE ULIPO.**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

Juma Waziri ameleta maombi yake dhidi yako mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Kilindi-Tanga lililopo Songe. Maombi haya yamepangwa kutajwa Tarehe 22/08/2022 saa tatu asubuhi mbele ya Mh.E.R Mhina Mwenyekiti.

Hivyo basi unatakiwa kufika wewe mwenyewe au wakili wako kwa tarehe Iliyopangwa, Vielelezo kuhusu shauri hili vinapatikana katika masijala ya wazi la Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Kilindi, Endapo hautahudhuria/hautafika shauri Hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila uwepo wako.

**Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kilindi leo tarehe 12/08/2022.**

MHINA ER
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KILINDI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA KIHONDA, MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na.51...2022**
**JINA LA MDAI: YOHANA AUGUSTINO**
**JINA LA MDAIWA: JASMIN JOHN**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:JASMIN JOHN WA KIHONDA MOROGORO**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Madai ya pesa shilingi 1350000/=.Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 15/08/2022 saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29/07/2022**

............................
HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA UBUNGO**
**LILILOPO KIBAMBA - LUGURUNI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 5 YA MWAKA 2017**
- **VIOLETH J. MKOMWA MUOMBAJI**
- **BEDA A. MLAUGWA**

**DHIDI YA**
**KELVIN DAVID MROPE**
**MICHAEL HASSAN MROPE**
**......WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**KELVIN DAVID MROPE NA MICHAEL HASSAN MROPE**
**POPOTE MLIPO**
**VIOLETH J.MKOMWA NA BEDA A MLANGWA**
Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) UBUNGO lililopo Luguruni/Kibamba Maombi hayo Yamepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 22/8/2022 SAA TATU ASUBUHI
Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa.
Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi wa Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo Endapo hamtatekeleza/hautatekeleza maombi haya yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 12/8/2022

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**(W) – UBUNGO**
**DAR ES SALAAM**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JASMIN ABDALLAH SHEMOKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P2540-0016** kilichotolewa na **ITEBWA SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/320559/2022.**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-18

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Walishikana mikono kama wapenzi waliopotezana kwa muda mrefu, wakaingia ndani, kila mmoja akiwa na furaha tele, akitaka kujua nini kilitokea baada ya kutoonana machoni kwa mwaka mzima.

Kesho yake Siwatu alimsimulia kile kilichotokea pale. Kuanzia kubakwa na mtu asiyejulikana, kuokota leso chini ya kitanda ambayo ilidaiwa kuwa ni ya kijana mmoja kijijini hapo aitwaye Maiko, na hata uongozi wa kijiji kumtuhumu yeye ndiye aliyefanya kitendo hicho.

Siwatu na Bakari hawafichani kitu japo hawakuwahi kuwa wapenzi, alimfahamisha pia mpaka jinsi ambavyo ameposwa.

“Mhh umepata mchumba?”

“We acha tu, nimekataa barua za wachumba wawili. Hii ya tatu nimeshindwa mwenzangu, maana wewe ulivyokuwa hapa kidogo ulikuwa unanipa kampani, hata wakinizodoa nina wewe, leo hii haupo, nimekuwa mpweke sana, nimekomaa weee, mpaka nimeamua kusalimu amri, nimekubali kuolewa.” Siwatu akajibu akimtazama Bakari usoni.

“Kwa hiyo ulinisubiri nije nikuoe mimi?” Akauliza swali tata ambalo lilimchanganya kidogo Siwatu.

Mtu ambaye hawajawahi kuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi, zaidi ya kaka na dada, leo anaongea maneno haya?

“Tuache hayo, na huyo aliyekubaka, nikasingiziwa mimi?”

“Nimeamua kuacha tu mwaya, maana kuna mambo kijijini hapa, we acha tu”

“Hapana Siwatu, kwa sababu limenihusisha mimi, naomba unipe mimi hiyo leso, halafu nitajua la kufanya.”

“Kwani unataka kufanya nini?”

“Nitajua, ila nataka nijisafishe kwenye kijiji chenu. Nataka niwaambie mimi siyo mbakaji. Hivi ni kweli nimekubaka mimi?” Akauliza kwa utani.

Siwatu akacheka. “Hata mimi niliwauliza hivyo hivyo. Wana wazimu, si wao wenyewe walikuwa wanasema mimi na wewe ni wapenzi? Sasa kwa nini leo tena waseme eti ulikuja usiku ukanibaka. Lakini najua ni kwa sababu niliwaambia wewe hukuwa mpenzi wangu, ulikuwa unalala chini mimi kitandani, hatukuwahi kufanya chochote, ndiyo maana wakachukulia hiyo faida.”

“Sasa ndiyo nataka niwaonyeshe nani alifanya jambo hilo la kikatili, pole sana mama.”




**Alichofanya Siwatu ni kumfuata Bakari alipokuwa amekaa, akamkubatia, machozi yakamtoka.**

“Ahsante.”

“Nimekuja hapa kukaa wiki moja tu. Nimekujaa maalumu kwa ajili ya kuja kukusalimia. Kukaa na wewe kwa wiki hii ili kurudisha upendo wote ambao umenifanyia, tangu uliponioana nikiwa nimejeruhiwa, nimetupwa porini, ukalazimishwa nichukuliwe, ukanihifadhi licha ya kupata upinzani mkali. Wewe unastahili tunu, taji na wala si haya ambayo tangu niondoke yamekuwa yakikupata Siwatu wangu.”

“Mhh, sijui niseme nini nashukuru sana Bakari wangu.” Siwatu alisema kwa sauti ya kutia huruma.

“Kwanza kabisa wakati ule tulipokuwa tunakwenda shamba, kuna lingine pale pembeni la mzee Tamasha alikuwa analiuza, limeshanunuliwa?”

“Bado.”

“Basi nitatoa pesa ili ulinunue uliunganishe lote liwe lako.” Siwatu alitoa macho kwa mashangao aliposikia maneno hayo.

Shamba lake ni heka mbili, aliloachiwa na wazazi wake, lakini la mzee Tamasha ni heka nne.

Hata kama ni wema alioufanya, lakini aliona kama mwenzake amekuja na kitu kipya zaidi.

Kabla hajashukuru wakati anashangaa, Bakari akaendelea.

Mwisho shamba la mzee Tamasha, mita kadhaa kuna mto umepita, nitakachofanya ni kutafuta wataalam ili wachimbe mfereji hadi kwenye shamba lako, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, lengo ni kwamba kifanyike kilimo cha mwagiliaji ambacho hakina msimu, unavuna na kupanda tena. Kwa hiyo hata mpunga pale unaweza kuliwa.”

Siwatu hakujua la kusema wala la kufanya. Alichanganyikiwa kwa furaha. Ni vitu ambavyo aliviona kwake kama ndoto.

“Na vile vile kuanzia sasa hutolima tena kwa mikono kama tulivyokuwa tunafanya, au kukodisha vibarua. Kila mwaka nitaleta trekta kwa ajili ya kulima shamba lako kwa sababu sasa nimeshakuwa na hekari sita na si mbili tena.”

Alichofanya Siwatu ni kumfuata Bakari alipokuwa amekaa, akamkubatia, machozi yakamtoka.

“Bakari wangu umenivika nguo. Nimetoka sehemu moja na kwenda nyingine kwa muda mfupi tu. Sikutegemea kama nitaweza kulimisha kwa trekta, au kuwa na shamba la hekari sita. Nadhani kama nitalima na kuuza kama inavyotarajia, kwa miaka mitatu tu sitakuwa hivi. Kwani Bakari uwezo wote huo umeupata wapi kwa muda huu mfupi? Mbona ulivyotoka hapa hukuwa hivyo? Umepata kazi wapi na kuweza kufanya yote hayo yanayohitaji gharama kubwa sana?”

“Siwatu, kabla sijakwambia hilo, kuna jambo lingine naomba nikwambie kwanza, ili tuje huko.”

“Nini tena Bakari?”

“Najua hapa umeniambia kuwa kuna barua ya uchumba imekuja. Kuna mtu anataka kukuoa, sawa?”

Siwatu akashtuka, akamwangalia Bakari usoni kwa makini, halafu akajibu.

“Ndiyo.”

“Mimi pia nawasilisha ombi langu la kutaka kukuoa.”

“Kunioa?” Akauliza kwa mshangao.

“Ndiyo.” Bakari akajibu kwa msisitizo.

Siwatu alichoka. Kichwa kikaanza kumuuma. Mtu aliyeishi naye, akalala naye chini ya paa moja kwa miezi mitatu, hajawahi kumtamkia neno lolote la kumhitaji. Alilala chini na yeye kitandani. Licha ya wanakijiji wengi kutokubaliana na hilo, na kujua kabisa kuwa ni mtu na mpenzi wake licha ya wenyewe kukanusha, leo hii anamtamkia kuwa anataka kumuoa.

Walikuwa wanapendana sana na bado wanapendana, lakini hawakuwahi kuambiana neno lolote la mapenzi hadi Bakari anaondoka, licha ya kwamba miili na macho yao yalionekana kuhitajiana.

Siwatu alionekana kutoshangaa, Bakari kumpenda, lakini alichoshangaa na kushtuka kuwa maneno yale yamechelewa sana. Angeambiwa tangu kipindi kile ambacho anaishi kijijini pale wala asingepinga.

Na mpaka sasa bado Siwatu anampenda sana Bakari licha ya kwamba hawaambiani. Lakini tayari ameshakubali kuolewa na mwanaume mwingine.

“Bakari, mbona unanitia kwenye majaribu? Mbona unanipa majanga? Kwanini usingeniambia mapema kabla hujaondoka? Mimi nimekataa wanaume wengi tu, nisingeshindwa kumkataa huyu ambaye simtambui. Ningekusubiri hata miaka miwili. Ni kweli Bakari mimi nakupenda sana, lakini nimeshakubali kuolewa na mtu mwingine. Hapa unanipa majaribu upya, furaha yangu yote imepotea.” Akalalamika mtoto wa watu.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# RAGE: BEKI SIMBA KAMILI, YANGA BADO

Na Hadija Mngwai

ALIYEWAHI kuwa Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Ismail Aden Rage, amezichambua timu kongwe zinazovaana leo kwa kusema Simba ipo vizuri kwa upande wa beki na washambuliaji, huku Yanga ikiwa haijakaa sawa upande wa beki.

Simba na Yanga zinashuka dimbani leo uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam katika mchezo wa Ngao ya Jamii ukiwa ni ufunguzi wa ligi kuu msimu wa 2022/23.

Akizungumza na Nipashe, Rage amesema kuwa, kwa jinsi alivyoviona vikosi vyote viwili licha ya kufanya usajili mzuri amebaini beki ya Yanga kutokuwa vizuri zaidi ya Simba licha ya kuwa na kikosi kizuri.

"Mechi ya leo itakuwa ngumu kutokana na usajili wa timu zote mbili ulivyofanywa, mara nyingi huwa ni nyepesi kutabiri mshindi, lakini mechi ya kesho ' leo' ni ngumu kutabiri kwa sababu mbili.

"Moja timu zote mbili zimesajili vizuri, pili wanao wachezaji wazuri lakini niseme wazi si kwa ushabiki naweza kutoa 'advantage' kwa Simba ambao wamesajili washambuliaji wazuri na beki ipo vizuri pia kwa jinsi nilivyoiona ikicheza mechi ya kirafiki dhidi ya St. George.

"Yanga yenyewe ina kikosi kizuri sana kwa upande wa washambuliaji, lakini beki haipo sawa kutokana na mechi walizocheza ukiangalia ile ya mwisho dhidi ya Coastal Union na hii dhidi ya Vipers ya Uganda ambayo walifungwa 2-0.

"Mara nyingi mechi za Simba na Yanga huwezi kuzitabiri nani anaweza kushinda lakini natoa nafasi kubwa kwa Simba," alisema Rage.



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hasan Elias Masalla (katikati mwenye suti) akiwa katika picha ya pamoja na manahodha wa timu 20 zitakazoshiriki mashindano ya The Angeline Ilemela Jimbo Cup 2022. Michuano hiyo imeandaliwa na Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dk Angeline Mabula. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Meneja adai uwanja Sokoine uko vizuri

Na Adam Fungamwango

BAADA ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, TFF, kuvifungia uwanja vitano kutumika kwenye mechi za Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza Agosti 15 kutokana na kutokidhi vigezo, huku vitatu ukiwemo wa Sokoine jijini Mbeya vikiwa kwenye uangalizi maalum, meneja wa uwanja huo, Modestus Mwaruka ameibuka na kudai kwa sasa umefanyiwa ukarabati wa kutosha, licha ya kubaki vitu vichache tu, hivyo kuiomba Bodi ya Ligi kwenda kufanya ukaguzi kabla ya kuuruhusu.

Akizungumza kutoka Jijini Mbeya, Mwaruka alisema ungeweza kutumia hata Agosti 15 kwa sababu asilimia kubwa ya mapungufu yaliyoanishwa wameyafanyia kazi na kilichobaki ni kuweka nyavu mpya golini pamoja na kufanya usajili wa jumla.

"Walituambia uwanja haupo sawa, una mabonde mabonde, tumeweka michanga sehemu ambazo zina mabonde ili kusawazisha, tumeshindilia, lakini changamoto nyingine ilikuwa ni vyumba vya kuvalia, kulikuwa na tatizo kwenye taa, tayari tumeshaweka mpya, yaliyobaki sasa ni marekebisho madogo tu, kuweka vyavu mpya na kufanya usafi wa jumla. Kwa jinsi ambavyo tumefikia ingewezekana hata Agosti 15 ligi inapoanza uwanja utumike, lakini tutarajia kuwa utaanza kutumia Septemba 9 kwenye mechi kati ya Mbeya City na Prisons," alisema Mwaruka.

Pia meneja huyo amezikaribisha timu zingine ambazo zinataka kuutumia uwanja huo pale utakapokuwa umefunguliwa kufanya hivyo na watakuwa tayari kushirikiana nazo, huku akiitaka Bodi ya Ligi kutuma waangalizi wake haraka ili kukiruhusu kutumia kwenye ligi baada ya kufanyiwa maboresho.

Uwanja wa Sokoine upo kwenye orodha ya viwanja ambayo vipo kwenye uangalizi maalumu kutokama na kuwa kwenye maboresho, pamoja na Majaliwa, Ruangwa Lindi na Katiba, Bukoba mkoani Kagera.

Viwanja vilivyosimamishwa kabisa ni Mkwakwani Tanga, Nyankumbu Girls ya Geita, Ushirika Moshi, Mabatini Mlandizi mkoani Pwani na Jamhuri Dodoma.

# Katwila: Ihefu itafanya kweli Ligi Kuu

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Zuber Katwila amedai usajili mzuri waliofanya pamoja na maboresho ya kikosi chake ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ihefu imepanda daraja kwa mara ya pili kushiriki Ligi hiyo baada ya msimu uliopita kufanikiwa kumaliza kuwa Mabingwa wa Ligi ya Championship.

Akizungumza na gazeti hilo jijini jana, Katwila alisema anajivunia usajili wa wachezaji wapya kwa kusajili wachezaji wenye uzoefu mkubwa katika Ligi hiyo, ikiwemo beki wa kimataifa Nicholas Wadada, Never Tigere na Papy Tshishimbi.

Alisema mbali na nyota hao kuna wachezaji wengine ambao wamewasajili kwa ajili ya kuboresha kikosi chao na kutarajia makubwa kutoka kwao ikiwemo kufikia malengo yao ya kushindana na kuleta changamoto katika ligi hiyo.

"Maandalizi yapo vizuri tunaendelea kufanyia kazi yale madhaifu yetu tuliyoyaona katika michezo yetu ya kirafikia, tukianzia safu ya ulinzi, viungo na washambulia kuifanya inakuwa imara na tunaenda kushindana kutafuta matokeo mazuri katika kila mechi," alisema Katwila.

Alisema kuboresha kikosi chao hasa kusajili wachezaji wakigeni kwao ni zana kubwa ambyao inawapa matumaini ya kufanya vizuri kwa msimu mpya wa ligi hiyo inayotarajia kuanza rasmi wiki ijayo.

Ihefu watafungua pazi la ligi hiyo akiwakaribisha Namungo FC, mchezo utakaopigwa katika Agosti 19, mwaka huu katika uwanja wa Estate Highland uliopo Mbeya.

# Chaneta yaitambia Afrika Kusini netiboli

Na Shufaa Lyimo

MJUMBE wa Kamati ya utendaji wa Chama cha netiboli Tanzania (Chaneta), Shukuru Kiwege amesema, wamejipanga vizuri kukutana na timu ya Afrika Kusini ambayo wataanza nayo kwenye mashindano ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Agosti 21 mwaka huu Pretoria nchini Afrika Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana mjumbe huyo alisema waneiona ratiba ya mashindano hayo na kudai hakuna timu wanayoihofia katika kundi lao.

"Tumeona ratiba ipo vizuri hakuna timu ambayo tunaihofia kwani hata sisi tumejipanga vizuri kuipeperusha vema bendera ya Tanzania," alisema Kiwege.

Alisema wachezaji wanaendelea na mazoezi mazuri ambayo anaamini yatawasaidia kufanya vizuri kwenye mashindano hayo.

Alisema ni mashindano ambayo yanatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila nchi itakayoshiriki.

Ratiba hiyo imepanga makundi mawili ambapo kundi A zipo timu za Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe, Botswana pamoja na Tanzania.

Kwa upande wa kundi B ni Uganda, Malawi, Zambia, Kenya na Eswatini.

## ZISIKUPITE

### PSG WAMTAKA RASHFORD

KLABU ya Paris St-Germain ipo kwenye mazungumzo na wawakilishi wa Marcus Rashford kuhusu uwezekano wa kumsajili mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 24 kutoka Manchester United. (***L'Equipe - kwa Kifaransa***)

### RABIOT KIKAO NA MAN

MANCHESTER United pia wana mkutano ulioratibiwa na mamake, Adrien Rabiot na wakala wake baada ya kukubaliana ada na Juventus kumnunua kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27. (***Fabrizio Romano***).

### LODI AWANIWA

KLABU ya Manchester City ina nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Atletico Madrid na Brazil, Renan Lodi mwenye umri wa miaka 24. (***Telegraph***)

### TIERNEY ATAKIWA

MLINZI wa kushoto wa Arsenal, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 25, pia ni miongoni mwa majina kwenye orodha ya wanaowania Manchester City. (***90 Minutes***)

### AUBAMEYANG HATAKI KURUDI

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33, angependelea kusalia Barcelona kuliko kurejea katika Ligi ya England pale Chelsea. (***Sport, via Metro***)

### DENNIS ATAKIWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imewasilisha ombi la kwanza kwa mshambuliaji wa Watford na Nigeria, Emmanuel Dennis mwenye umri wa miaka 24. (***The Athletic***)

### PALMIERI AGOMBEWA

KLABU ya Atlanta itachuana na Nottingham Forest katika kumsajili winga wa Italia, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 28 kutoka Chelsea. (***Standard***)

### GUIRASSY AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton inatarajia kukamilisha dili la kumsajili mshambuliaji wa Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 26 kutoka Rennes. (***L'Equipe***)

### ADAMS AWINDWA

CHE Adams wa Southampton ana nia ya kutaka kuhamia Everton, lakini kuna ushindani kutoka kwa Leeds United, Wolves na Nottingham Forest kwa mshambuliaji huyo wa Scotland mwenye umri wa miaka 26. (***Mail***).

### KALAJDZIC AKATAE

ALIYEKUWA kocha wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick amependekeza kwamba mshambuliaji wa Stuttgart na Austria, Sasa Kalajdzic mwenye umri wa miaka 25, anapaswa kukataa kuhamia Old Trafford. (***Star***)

### DEPAY ANUKIA JUVE

KLABU ya Juventus wanakaribia kukamilisha dili la kumnunua mshambuiaji wa Barcelona na Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28. (***90min***).

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN HAINA MPANGO KUMUUZA RASHFORD

## Mwenyewe ataka kubaki ili apiganie namba kikosi cha kwanza na...

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United haina nia ya kuachana na Marcus Rashford msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Mshambulizi huyo wa kimataifa wa England, Juni alibainisha nia yake ya kurejesha nafasi yake kwenye kikosi hicho pale Old Trafford na alikuwa anatazamia kufanya kazi chini ya Ten Hag na Steve McClaren, ambao wote wawili wanajulikana kuwa mashabiki wake.

Wawili hao wamezungumza na Rashford kuhusu jukumu lake katika timu na mustakabali wake United, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ana furaha kufanya kazi chini ya Ten Hag na McClaren.

Rashford amebakiza chini ya mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa - ingawa United wana chaguo la kuongeza kwa miezi 12.

**Lakini kwa mujibu wa 90min, klabu ya Paris Saint-Germain imeonesha nia ya kuitaka saini ya mchezaji huyo ingawa hakuna mawasiliano rasmi**

Lakini vyanzo vimeithibitishia 90min kwamba, Rashford hataruhusiwa kuondoka kwani United na yeye mwenyewe hana mpango wa kuondoka Old Trafford.

Kocha wa PSG, Christophe Galtier aliyeteuliwa msimu huu kuchukua nafasi ya aliyekuwa kocha mlengwa wa United, Mauricio Pochettino, amethibitisha nia yake ya kusajili fowadi mpya, licha ya kumuongeza Hugo Ekitike kwenye kikosi chake kwa mkataba wa mkopo wa msimu mzima kutoka Reims.

Kuhusu Rashford, anaangazia kuanza mara kwa mara kwenye kikosi cha United kwa mara nyingine, ambayo inaweza kusaidia nafasi yake ya kulazimisha kurudi kwenye kikosi cha Gareth Southgate cha England kabla ya Kombe la Dunia.

Rashford alicheza dakika zote 90 za mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya United dhidi ya Brighton, akianzia winga ya kushoto huku Mashetani Wekundu wakichapwa mabao 2-1.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,021,2
MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
SIMBA SC
1 | 2.50
X | 2.80
2 | 2.75
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TIERNEY WA ARSENAL AWINDWA MAN CITY



**LONDON,** England

KLABU ya Manchester City inataka kusajili mlinzi mpya wa kushoto msimu huu wa joto, huku 90min ikithibitisha kwamba, Kieran Tierney wa Arsenal ni miongoni mwa majina yaliyopo kwenye orodha yao fupi.

Kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kilijaribu kumsajili Marc Cucurella mwanzoni mwa msimu huu wa joto, lakini kilishindwa kufikia bei yake ya pauni milioni 55 na badala yake akijiunga na Chelsea, na kuwaacha bila beki wa kushoto anayetambulika baada ya kuondoka kwa Oleksandr Zinchenko aliyekwenda Arsenal.

City wanaangalia chaguzi nyingi na vyanzo vimethibitisha kwamba, Tierney ni kati ya majina ambayo yamejadiliwa kule kwenye dimba la Etihad.

Uzoefu wa Tierney kwenye Ligi Kuu ya England unathaminiwa sana na Guardiola, lakini Arsenal hawataki kuachana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland, licha ya kumsajili Zinchenko mapema msimu huu wa joto.

Zinchenko ameanza msimu katika nafasi ya beki wa kushoto huku Tierney akikosekana kwa sababu ya majeraha, lakini mpango wa Arsenal mara zote umekuwa ni kumpa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ukraine dakika katika nafasi anayopendelea ya kiungo.

Wakijua kwamba dili la Tierney lingekuwa gumu sana - na ghali - kuliondoa, City imekuwa ikiangalia pia walinzi wengine.

Alex Grimaldo wa Benfica, ambaye zamani alikuwa analengwa na Arsenal, pia anazingatiwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England, huku City pia wakipewa nafasi ya kumsajili Renan Lodi wa Atletico Madrid msimu huu wa joto.

# Aguero atashangaa City ikimwacha Silva



**MANCHESTER,** England

SERGIO Aguero atashangaa iwapo Bernardo Silva ataondoka Manchester City na kwenda Barcelona, lakini anaamini kuwa kiungo huyo anaweza kuwa na mchango mkubwa katika kumjenga Xavi iwapo uhamisho utapitishwa.

Barca tayari imewasajili Robert Lewandowski, Raphinha, Jules Kounde, Andreas Christensen na Franck Kessie.

Huku Frenkie de Jong akitarajiwa kuondoka pale Camp Nou, ripoti zimesema mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Silva ndiye anayelengwa zaidi na Xavi.

Silva aliichezea City mechi 50 katika michuano yote msimu uliopita, idadi hiyo ilipitwa na Joao Cancelo pekee (52), akifunga mabao 13 na kutoa asisti saba.

Ni Kevin de Bruyne (129) na Jack Grealish (78) pekee waliotengeneza nafasi nyingi kwa City kuliko 76 za Silva msimu uliopita, lakini anaweza kusonga mbele baada ya kusema mabingwa hao wa Ligi Kuu England "wanajua ninachotaka" wiki hii.

Aguero - mchezaji mwenzake wa zamani na Silva kabla ya kuondoka City na kwenda Barcelona 2021 - hana uhakika kama uhamisho huo utatimia, lakini anaamini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atamfaa zaidi Xavi.

"Bernardo ni mchezaji mzuri. Anabeba mpira, anajitolea, ana ubora wa kusaidia na kufunga mabao na anaweza kucheza katika nafasi tofauti," alisema Aguero akiiambia Sky Sport.

"Itanishangaza ikiwa City itamwacha aondoke, ni mchezaji anayechangia sana kila msimu, lakini kila kitu kinawezekana.

"Ikiwa hatimaye atawasili Barca, basi atakuwa mtu ambaye anaweza kuwa muhimu kwa mchezo wa kumiliki mpira ambao Xavi anapenda."

## HABARI MICHEZO


208,577/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/2022 | 17:00 | Brighton vs Newcastle | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 02. 13/08/2022 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.24 | 3.39 | 3.09 |
| 03. 13/08/2022 | 17:00 | Wolverhampton vs Fulham | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 04. 13/08/2022 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 05. 13/08/2022 | 17:00 | Sunderland vs QPR | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 06. 13/08/2022 | 17:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.28 | 2.98 |
| 07. 13/08/2022 | 21:45 | AC Monza Brianz vs Torino | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 08. 14/08/2022 | 13:15 | FC Volendam vs NEC Nijmegen | 2.53 | 3.47 | 2.63 |
| 09. 14/08/2022 | 15:00 | Viborg FF vs Silkeborg IF | 2.83 | 3.48 | 2.36 |
| 10. 14/08/2022 | 16:00 | Middlesbrough vs Sheffield Utd | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 11. 14/08/2022 | 16:00 | Troyes vs Toulouse | 2.58 | 3.17 | 2.73 |
| 12. 14/08/2022 | 16:00 | AJ Auxerre vs Angers | 2.28 | 3.11 | 3.21 |
| 13. 14/08/2022 | 16:30 | Mainz vs Union Berlin | 2.29 | 3.26 | 3.06 |
| 14. 14/08/2022 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.41 | 3.29 | 2.89 |
| 15. 14/08/2022 | 18:05 | Nice vs Strasbourg | 2.23 | 3.21 | 3.21 |
| 16. 14/08/2022 | 18:30 | Chelsea vs Tottenham | 2.22 | 3.33 | 3.18 |
| 17. 14/08/2022 | 18:30 | Cadiz CF vs Real Sociedad | 3.13 | 3.13 | 2.35 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 13 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1814 | Aston Villa vs Everton | 1.77 | 3.44 | 4.49 |
| 14:30 | 3247 | Cardiff vs Birmingham | 2.24 | 3.16 | 3.16 |
| 15:00 | 3379 | Lokomotiv Moscow vs Kryliya Sovetov | 2.32 | 3.41 | 2.81 |
| 16:30 | 1650 | Bayer Leverkusen vs Augsburg | 1.30 | 5.40 | 8.00 |
| 16:30 | 1775 | Hoffenheim vs VfL Bochum | 1.55 | 4.29 | 4.99 |
| 16:30 | 4146 | Hertha BSC vs Eintracht Frankfurt | 2.91 | 3.36 | 2.28 |
| 16:30 | 4446 | Werder Bremen vs Stuttgart | 2.27 | 3.45 | 2.85 |
| 16:30 | 5360 | RB Leipzig vs FC Koln | 1.43 | 4.59 | 6.19 |
| 17:00 | 1400 | Rotherham vs Reading | 2.16 | 3.30 | 3.20 |
| 17:00 | 2033 | Wigan vs Bristol City | 2.15 | 3.30 | 3.20 |
| 17:00 | 2094 | St Mirren vs Ross County | 2.33 | 3.17 | 3.02 |
| 17:00 | 2408 | Arsenal vs Leicester | 1.55 | 4.05 | 5.28 |
| 17:00 | 2596 | Manchester City vs Bournemouth | 1.09 | 8.04 | 24.59 |
| 17:00 | 3230 | Zenit St Petersburg vs CSKA Moscow | 1.51 | 4.28 | 5.38 |
| 17:00 | 3250 | KVC Westerlo vs Standard Liege | 2.07 | 3.31 | 3.46 |
| 17:00 | 3357 | Livingston vs Hibernian | 2.97 | 3.02 | 2.46 |
| 17:00 | 3464 | Hull City vs Norwich City | 3.39 | 3.39 | 2.04 |
| 17:00 | 3482 | Blackpool vs Swansea | 2.33 | 3.26 | 2.90 |
| 17:00 | 3579 | Millwall vs Coventry | 2.38 | 3.10 | 2.95 |
| 17:00 | 3595 | Brighton vs Newcastle | 2.37 | 3.14 | 2.94 |
| 17:00 | 3731 | Rangers vs St Johnstone | 1.18 | 6.24 | 15.11 |
| 17:00 | 4014 | Huddersfield vs Stoke City | 2.66 | 3.11 | 2.61 |
| 17:00 | 4120 | Luton Town vs Preston | 2.23 | 3.25 | 3.10 |
| 17:00 | 4611 | Sunderland vs QPR | 2.09 | 3.40 | 3.25 |
| 17:00 | 5150 | Wolverhampton vs Fulham | 2.31 | 3.20 | 3.00 |
| 17:00 | 5316 | Southampton vs Leeds | 2.23 | 3.35 | 3.00 |
| 17:00 | 5626 | Aberdeen vs Motherwell | 1.78 | 3.42 | 4.53 |
| 18:00 | 2317 | Monaco vs Rennes | 2.17 | 3.48 | 3.07 |
| 18:00 | 5235 | Celta Vigo vs Espanyol | 1.84 | 3.59 | 4.04 |
| 19:00 | 1576 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.06 | 3.48 | 3.32 |
| 19:00 | 5223 | Young Africans vs Simba | 2.50 | 2.80 | 2.75 |
| 19:15 | 2361 | Cercle Brugge vs Mechelen | 2.07 | 3.46 | 3.31 |
| 19:30 | 1313 | Schalke 04 vs Monchengladbach | 2.96 | 3.61 | 2.15 |
| 19:30 | 2580 | AC Milan vs Udinese | 1.39 | 4.60 | 7.00 |
| 19:30 | 3807 | Brentford vs Manchester Utd | 3.47 | 3.34 | 2.03 |
| 19:30 | 4269 | Sampdoria vs Atalanta | 4.11 | 3.81 | 1.74 |
| 19:45 | 4461 | GO Ahead Eagles vs PSV Eindhoven | 7.40 | 4.90 | 1.35 |
| 20:00 | 3984 | Valladolid vs Villarreal | 3.78 | 3.53 | 1.92 |
| 20:00 | 4363 | Dinamo Moscow vs FC Krasnodar | 1.81 | 3.70 | 3.90 |
| 20:00 | 5822 | Casa Pia Atletico vs Benfica | 11.01 | 5.81 | 1.23 |
| 21:00 | 2287 | Emmen vs Waalwick | 1.93 | 3.51 | 3.61 |
| 21:00 | 2421 | Utrecht vs Cambuur | 1.46 | 4.60 | 5.60 |
| 21:30 | 4238 | St. Gallen vs FC Luzern | 2.01 | 3.67 | 3.27 |
| 21:45 | 2130 | Lecce vs Inter | 8.98 | 5.39 | 1.28 |
| 21:45 | 4033 | Monza vs Torino | 2.51 | 3.21 | 2.71 |
| 21:45 | 5942 | Galatasaray vs Giresunspor | 1.43 | 4.41 | 6.62 |
| 22:00 | 1190 | Paris St Germain vs Montpellier | 1.12 | 8.12 | 16.08 |
| 22:00 | 1245 | Feyenoord vs Heerenveen | 1.28 | 5.58 | 8.17 |
| 22:00 | 2428 | Barcelona vs Rayo Vallecano | 1.24 | 5.80 | 10.87 |
| 22:30 | 4945 | Sporting Lisbon vs Rio Ave | 1.21 | 5.80 | 13.01 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# RUVU SHOOTING KIDEDEA ZANZIBAR PRE SEASON

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Ruvu shooting ya Tanzania bara imefanikiwa kunyakuwa Ubingwa wa Michuano ya Kombe la Zanzibar (Pre season Tournament) lililoandaliwa na kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar, ZFF.

Ruvu Shooting imetwaa ubingwa huo baada ya kuwachapa Mabingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar KMKM bao 1-0 katika mchezo wa fainali wa michuano hiyo uliopigwa juzi dimba la Amaan.

Bao hilo la Ruvu liliwekwa kimiani na mchezaji, Samsoni Kwakwala katika dakika ya 79.

Akizungumza na waandishi wa habari Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai juu ya mashindano hayo alisema lengo la ZFF kuwa na mashindano mengine kwa klabu limefanikiwa kama walivyotarajia.

Alisema ZFF imebuni mashindano haya ili kuzisaidia klabu za Zanzibar kupata mapumziko mazuri ya msimu kwa kuwapima wachezaji wao katika michezo yenye ushindani.

"Lengo letu kwa asilimia kubwa tumefanikiwa, nia yetu kubwa ni kuzisaidia klabu zetu na tunajua uwezo wao wa kifedha hazimudu kuweka kambi nje ya nchi. Sasa mashindano haya yatawasaidia hata kuujua vizuri usajili wao mpya.

Mashindano ya Zanzibar Pre season Tournament yalishirikisha timu nne ambazo ni KMKM, Kipanga, Kundema pamoja na Ruvu Shooting kutoka Tanzania bara.



Wachezaji na viongozi wa Ruvu Shooting wakishangilia ubingwa wao. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Malkia wa mipasho mbioni kufyatua tano kwa mpigo

**Na Sabato Kasika**

MALKIA wa mipasho nchini, Khadija Kopa, amesema yuko mbioni kufyatua nyimbo tano kwa mpigo, ikiwa ni mwendelezo wa kuandaa albamu yake mpya kwa mwaka huu wa 2022.

Kopa alisema hayo wakati akihojiwa na kituo kimoja cha redio, jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa kimya kingi kina mshindo mkuu, na kuwataka mashabiki wake kujiandaa kupata vitu vipya.

"Mashabiki wangu ninawaambia kuwa nipo, na wakati wowote nitatoa nyimbo mpya tano kwa pamoja, hivyo jiandaeni kusikia vitu vipya kutoka kwa Malkia wa mipasho," alisema Kopa. Mbali na kufyatua nyimbo tano, mkongwe amewashauri wasanii wapya wa muziki wa taarab kuwa na heshima kwa wakubwa wao, kwa madai kwamba, bila kufanya hivyo hawawezi 'kutoboa' kwenye sanaa.

"Kila ninapokutana na wasanii wa kike huwa ninawashauri na kuwapa moyo kuhusu maisha ya muziki, kwani vijana wetu wengi wa sasa hivi hawana busara kusema ngoja nimfuate mtu mzima atanielekeza njia za kupita," alisema.

Kopa amesema wengi wanajifanya wanajua, hali ambayo hujikuta wakipotea mapema kwenye sanaa, huku yeye mkongwe akiendelea kufanya vizuri kwenye muziki huo hadi sasa.

Mkongwe huyo alitoa siri ya yeye kuendelea kudumu kwenye gemu kwa muda mrefu kuwa ni kutokana na kuongea vizuri na wale aliowakuta kwenye gemu na kupokea ushauri wao na kuufanyia kazi.

"Lakini leo mtu anaingia kwenye taarab tu na kuanza kupandisha mabega juu na kujifanya anajua kuliko wale aliowakuta. Kwa hali kama hiyo si rahisi msanii mchanga kutoboa, heshima ni ya muhimu," amesema.

Ameongezaa kuwa watu wengi huwa wanamuogopa, wakidhani kwamba ni mkali na kumbe ni wa kawaida na mtu poa, ambapo amewataka wale wanaohitaji ushauri kutoka kwake wamfuate bila hofu.

# Michezo

Nipashe Jumamosi Agosti 13, 2022




Man haina mpango kumuuza Rashford

UKURASA 21



Stephane Aziz Ki



Nelson Okwa

# Lazima tuwachape

## Ni Yanga dhidi ya Simba kwenye Ngao ya jamii leo, Manula, Kambole nje ...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KUELEKEA mchezo wa Ngao ya Jamii utakaopigwa leo makocha wa timu zote mbili Yanga na Simba wametamba kila mmoja kuibuka na ushindi na kuondoka na taji hilo.

Mchezo huo unachezwa leo saa 1:00 usiku, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku Yanga wakiwa wenyeji.

Katika mchezo huo mwamuzi wa kati atakuwa ni Heri Sasii, kutoka Dar es Salaam, akisaidiana na Mohamed Mkono kutoka Tanga na Kassim Mpanga (Dar es Salaam) na mwamuzi wa akiba ni Ramadhani Kayoko (Dar es Salaam).

Akizungumza jana Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki, alisema kuwa wamejiandaa vizuri kwani mchezo huo ni mkubwa ambao utaamuliwa na wachezaji wakubwa ingawa ni wa kawaida kama mingine.

"Mchezo ni dakika 90 timu yangu iko tayari kwa ajili ya mchezo tutashuhudia mechi nzuri na timu bora itapata matokeo mazuri," alisema Maki.

"Wachezaji wote wako vizuri ingawa tunaenda kumkosa Aishi Manula ambaye ana majeraha na hajafanya mazoezi na timu," alisema Maki.

Nahodha wa Simba John Bocco, alisema kuwa maandalizi ya mchezo huo ni mazuri wanaiheshimu Yanga, lakini kwa jinsi walivyojiandaa anaamini wanaenda kupata ushindi.

> **"Utakuwa mchezo mzuri tuna kikosi chenye wachezaji wazuri naomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kwani mechi hii itaenda kutoa taswira yetu ya msimu ujao," alisema Bocco.**

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema kuwa utakuwa mchezo mzuri wa kiufundi utakaokuwa ukifuatiliwa zaidi barani Afrika ingawa umekuja mapema zaidi katika kipindi cha maandalizi ya msimu mpya.

"Namkaribisha kocha Zoran na namtakia kila la heri kwenye mchezo huu, lakini pia nina furaha kwa kuwa kocha niliyefikisha michezo sita ya watani wa jadi," alisema Nabi. "Tumejiandaa vizuri ingawa mchezo huu umekuja mapema wachezaji wako kwenye hali nzuri tunaenda kumkosa Lazarous Kambole, ambaye alipata majeraha kwenye mchezo wa Namungo pamoja na Moloko ambaye kesho (leo) hatakuwa sehemu ya kikosi."

Nahodha wa Yanga, Bakari Nondo, alisema kuwa wao na benchi la ufundi wamejindaa vizuri kwa mchezo huo na anaamini wanaenda kutetea Ngao ya Jamii.

"Alisema kuwa matokeo yaliyopita hayawezi kuwatoa mchezoni na kuwataka mashabiki wa Yanga wajitokeze kwa wingi kwani wamepanga kuwashangaza," alisema Nondo.

Mechi ya leo inatarajiwa kuwa kali ya kusisimua kutokana na aina ya usajili ambao timu zote zimeufanya, huku baadhi ya wachezaji wakicheza 'dabi' hiyo kwa mara ya kwanza.

Simba ndiyo inayotarajia kuingia uwanjani na kuchezesha wachezaji wengi wapya kutokana na mapungufu waliyokuwa nayo msimu uliopita, tofauti na Yanga ambayo itakuwa inaziba tu baadhi ya mapengo ya msimu uliopita, lakini kwa asilimia kubwa ikitegemea kikosi kilekile.

Simba itakuwa na wachezaji wapya kama Augustine Okra, Vicent Akpan, Nelson Okra, Mohamed Ouattara na wengineo, huku Yanga ikiwa na kina Lazrous Kambole, Aziz Ki, Joyce Lomalisa, Gael Bigirimana na wengine.

Pia Yanga itakuwa na faida ya kuendelea kuwa na kocha wake wa msimu uliopita, Nabi wakati Simba ikiwa na kocha mpya, Maki mwenye uraia wa nchi za Ureno na Serbia.

Simba itataka kulipiza kisasi cha kufungwa kwenye Ngao ya Jamii msimu uliopita, ilipopata kipigo cha bao 1-0, Septemba 25 mwaka jana, likiwekwa wavuni na Fiston Mayele dakika ya 12 ya mchezo.

Tangu kuanza kwa Ngao ya Jamii, timu hizo zimekutana mara tano, Simba ikishinda mbili na Yanga mara tatu.

Mara ya kwanza ilikuwa ni 2001, Yanga ikishinda mabao 2-1 yaliyofungwa na Edibly Lunyamila na Ally Yusuph 'Tigana', huku bao la kufutia machozi la Simba likiwekwa wavuni na Steven Mapunda 'Garincha'.

2010 Yanga ilitwaa tena Ngao ya Jamii kwa kuifunga Simba kwa mikwaju 3-1 ya penalti, baada ya dakika 90 za suluhu, huku 2011, Simba ikishinda mabao 2-0 yaliyofungwa na Haruna Moshi 'Boban' na Felix Sunzu.

Simba ilifanikiwa ilichukua Ngao ya Jamii mbele ya Yanga 2017 kwa mikwaju 5-4 ya penalti, na mara ya mwisho ilikuwa mwaka jana, Yanga ikishinda bao 1-0.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >